
# SILAHA YA MUNGU





## KITABU CHA MWALIMU
kwa miaka yote

# SILAHA YA MUNGU

## KITABU CHA MWALIMU KWA MIAKA YOTE




**Mpango wa Shule ya Jumapili kutoka "Watoto ni Muhimu"**

**Wavuti: www.WatotoAreImportant.com/armour/**


### SHUKRANI KWA WOTE KATIKA TIMU YA "WATOTO NI MUHIMU"!

Mhariri Mkuu: Kristina Krauss
Timu ya Ubunifu: Abril Palacios Camacho, Areli Zuriel Salinas Sanchez, Dwight Krauss, Jacob Kuruvilla, Jennifer Sánchez Nieto, Julio Sánchez Nieto, Mike Kangas, Monserrat Duran Díaz, Rubén Darío, Suki Kangas, Verónica Toj, na Vickie Kangas.

Shukrani kwa Rubén Dario kwa muziki wa ajabu katika programu hii.
Timu ya Tafsiri: Ali Atuha, Aline Xavier, Annupama Wankhede, Anton Klymyk, Araz Mammadzadeh, Jarida la Machapisho na Vyombo vya habari, Arturo Jr Boron, Baraka Jacob, Carla Mayumi, Carmela Dawn Flores, Chrisbresnahan, David Raju, Ephraim Njuguna Mirobi, Finny Jacob, Geenav, HamidReza Azimi (hamid.azimi1364 kwa gm # ail com), Heyaudrey, I-clever.com, iqbalman, Jacob Kuruvilla, kamilturk, Karunguru Mwangi, kiran, Krauz1, Maitrayi Mondal, Marco Chu, Marcos Rocha, Mathew Das, Mitesh Mandaliya , mrramlama, BiGeethashree NavaneethaKrishnan, Nassim Bougtaia, nicbenk, Paul Mwangi, Paul Septan, Rana922, Rubina Rai, Sabrina Benny John, Safdar Khan, shahroshan15, SubtitleMe, Talento-Unido, ueritom, Verdia Juliusansohh Zeina Mirella Barzaga Arencibia.


### UTANGULIZI

Ndugu na Dada,
Kwa wakati huu tunakupandisha ngazi hadi sajenti katika jeshi la Mungu! Kila mtu katika kanisa lako atataka kushiriki katika nyenzo hii ya "Silaha ya Mungu". Wanaweza kuanza na nyenzo ya mkutano wa hadhara/siku ya mchezo iliyoundwa na ndugu kutoka Guatemala ambao ni Silvia Delio, Mario Velasquez na timu yake yote

ya usaidizi.Na kisha furaha hiyo itaendelea kwa sababu hawataweza kuacha kucheka kwa sababu ya michezo mipya ya kuigiza/michezo mifupi iliyobuniwa na Suki Kangas. Inafurahisha sana kusikia Jenny Sanchez akicheka wakati anahariri video ambazo Sagenti Mlingoti (Mike Kangas) na askari, Askari Mcheko (Suki Kangas) na Askari Zamu (Flor Boldo) wanapoigiza kwa furaha.Na kama michezo ya kuigiza ya Suki haikupi tabasamu, basi angalia muundo mpya wa kifurushi chote. Napenda jalada la kitabu cha mwalimu, likiwa na michoro yote ya kuchekesha, na Sajenti Mlingoti akijaribu kuwaza atafanya nini na askari hao wote! (Labda inalingana na darasa lako?)

Nina hakika kwamba mpango huu utawahimiza wanafunzi wako sio tu katika kukariri Silaha ya Mungu, lakini kuishi kulingana na mafunzo yake. Watoto watahamasishwa sana kupanda ngazi katika nafasi na kupata beji mpya za Suki, na watang'arishwa na beji hizi katika mabega yao. Sio watoto tu watakaotaka kushiriki lakini pia walimu, kwani Flor Boldo alibuni kwa ustadi sana.Nataka alamisho langu mwenyewe kwa Bibilia yangu! Vitabu vipya vya wanafunzi vinapendeza zaidi, vimeundwa na Monse Durán, kwa muundo na michoro mipya na msanii Douglas1985, na inaonekana kwamba hata walimu watatamani kupata kitabu cha kiwango cha juu zaidi ili kupata changamoto mpya!

Lakini mpango huu sio wa kufurahisha tu! Kuna ujumbe katika kila sehemu ya vitabu, kuanzia masomo mpya ambayo nimeandika hadi mada nzito katika sehemu ya maswali na majibu na kazi za ziada ya katikati mwa wiki zilizoundwa na Vickie Kangas. Na pia kuna ujumbe onaogusa roho moja kwa moja kupitia nyimbo, zote zilizoandikwa na Mike Kangas, hadi ujumbe wa kisasa wa WhatsApp katika upande wa nyuma wa vitabu ulioandikwa na Flor Boldo.

Kwa kugusia muziki, lazima nitamtaja kila mtu aliyeimba pamoja nami, kwa Kiingereza na Kihispania, ili nyimbo 10 za Silaha zipendeze, ziburudishe na ziwasiliane ujumbe mzito. Shukrani nyingi kwa Andy Kangas, Jessica Meshell na Austin Meshell kwa kunisaidia katika kubuni CD hiyo kwa Kiingereza na shukrani kwa Mike Kangas na Flor Boldo kwa kuimba pamoja nami kwa Kihispania. Lakini Suki alifanya nyimbo zipate msisimko ZAIDI kwa kutumia vitendo vyake vya ubunifu, na napendezwa zaidi na wakati ambapo timu nzima inatokea ikiwa ni pamoja na David, Julio, Flor, Monse, Jenny na Suki.

Kwa kweli, shughuli hii yote inafanikiwa kwa sababu ya kushirikiana, kuanzia wakati tulipoanza na maombi, hadi wakati Julio Sanchez alipomaliza kuchapisha maelezo ya mwisho kwa mauzo katika Mexico na Guatemala na hadi wakati Mike Kangas atakapopakia nyenzo za lugha zote kwenye wavuti ili uweze kuzipakua bila malipo. Na singependa kumsahau Verónica Toj kutoka Guatemala ambaye anasimamia Facebook na Baraka Jacob huko India ambaye anasimamia tafsiri katika India. Na shukrani nyingi kwa Flor Boldo kwa kunisaidia kuhariri kila kitu!

Hongera kwa timu yote, kwa kuboresha programu kwa kutumia upendo, ubunifu na huduma yenu. Pasipo kila mmoja wenu, singeweza kufanya chochote. Shukran pia kwa kila mwalimu katika mstari wa mbele wa vita, ambaye atakuwa akifunza madarasa haya na kuleta mabadiliko katika ulimwengu wetu. Hatubuni vitabu hivi ili visalie katika kabati lakini viweze kutoa mafunzo kwa kizazi kijacho. Bila ya uwepo wenu kama walimu, timu yetu haiwezi kufanikiwa. Asante kwa matunda ya kiroho mnayotupa kupitia upendo mlio nao kwa watoto, kujitolea na uvumilivu wenu.
Mungu abariki kila mmoja wenu maradufu!

Kristina Krauss
Watoto ni Muhimu

# JINSI YA KUTUMIA NYENZO HII

## UTOFAUTI



Student



Teacher

Kilicho bora zaidi na mpango huu ni alama za cheo/beji ambazo watoto na walimu wanaweza kupata.Kabla ya kuanza kila darasa, utataka kuandaa sherehe ndogo ya tuzo na kutoa beji. (Ikiwa hutaweza kukamilisha maandalizi kabla ya darasa, unaweza kufanya hivyo wakati wa nyimbo.) Kuna beji 4 za kushinda kila wiki. Kisha wanafunzi wanapowasili, andika maelezo ya kazi za nyumbani: sura zilizosomwa kutoka kitabu cha Matendo na kazi za "Kambi ya Mazoezi" ambapo walipaswa kufaya shughuli katikati ya wiki. Pia weka kumbukumbu ya mahudhurio yao ya kila wiki. Mwishowe, waombe wakueleze fungu la kumbukumbu (tutajifunza maandishi ya Silaha ya Mungu) ili waweze pia kupata nyota za ukariri. Weka kumbukumbu nzuri ya wale waliofanikiwa kupata alama za cheo na uweze kuzitoa rasmi kila wiki katika sherehe ndogo.

- Mahudhurio ya darasa
- Kazi ya nyumbani kuhusu maisha
- Kusoma kazi ya nyumbani
- Kukariri mafungu kuhusu Silaha

Kuna karatasi mwishoni mwa kitabu ambayo unaweza kutumia kurekodi alama zao za cheo.

## MAHUDHURIO

Kila mtoto anapata kipande cha beji kuu kwa kuhudhuria kila darasa. Unaweza kutoa beji 2 kwa kila mtoto ili avaea katika mikono yote miwili au 1 ya kuvaa katika mkono mmoja.




Mfano wa usaidizi wa sehemu, au siku chache tu. Weka mistari pamoja.



## KUSOMA NA KUKARIRI




Watoto wanaweza kupata nyota kwa kusoma sehemu ya kitabu cha Matendo iliyotengwa kwa kila somo na kupata nyota kwa kukariri fungu la siku. Ikiwa watasoma kitabu chote cha Matendo na kukariri mafungu 10, beji zao zitajaa. Weka beji hii katika upande wa kulia wa mtoto. (Beji ya Wiki ya 10 hupatikana ikiwa mwanafunzi amefaulu kupata beji katika madarasa 9 yaliyopita.)

## KAMBI YA MAZOEZI/SHUGHULI KUHUSU MAISHA

Kila somo pia lina shughuli ya kazi ya nyumbani ili kutumia somo katika maisha yao katikati mwa wiki.Watoto wanapata "riboni" (karatasi ya umbo la mstatili) baada ya kukamilisha kila shughuli. Unganisha mistatili na uzi, utepe au uigundishe pamoja na vipande vya karatasi. Iweke upande wa kushoto wa mtoto.



## RATIBA: (SAA 1 ½)

**(Dakika 10) Kabla ya darasa:**

- Watoto wanapowasili, andika mafanikio yao ili waweze kujipatia beji 4 kila wiki.
- Mahudhurio ya darasa
- Kazi ya nyumbani kuhusu maisha: "Kambi ya mazoezi"
- Kusoma kazi ya nyumbani: Kitabu cha Matendo
- Kukariri mafungu ya Silaha

**(Dakika 25) Ufunguzi:**

- Nyimbo zinazojumuisha vitendo
- Sherehe ya tuzo/ala za cheo
- Kichwa cha somo
- Mchezo wa kuigiza/Mchoro




**(Dakika 15) Somo:**

- Somo Kuu
- Fungu la Kumbukumbu

**(Dakika 20) Vitabu vya Wanafunzi:**

- Mafumbo na shughuli
- PowerPoint/Uamuzi
- Maswali/Majadiliano
- Tenga kazi ya nyumbani kuhusu maisha na kusoma

**(Dakika 20) Shughuli:**

- Mchezo
- Ufundi

## Michezo ya Kuigiza

Kila wiki, sajenti anawafundisha askari wawili kuhusu Silaha ya Mungu katika kambi ya mazoezi. Katika kila mchezo wa kuigiza, askari wapya wanajifunza somo linalofanana na somo la siku la shule ya Jumapili kwa watoto.



Wahusika:

• Askari Mcheko

Amechanganyikiwa na husahau vipande vya Silaha.

• Askari Zamu

Anajua kufuata maagizo.

• Sajenti Mlingoti

Ana jukumu la kutoa mafunzo kwa askari hao wawili.

Kwa nyenzo hii, tuna video za michezo yote ya kuigiza inayopatikana kwenye DVD au kwenye YouTube. Unaweza kutumia video ili kutoa motisha kwa wahusika wako halisi au unaweza kucheza video hizo moja kwa moja kwa watoto.

Video hizi za kuigiza hazitumii lugha halisi na zinaweza kutumika popote bila kujali lugha inayozungumzwa katika eneo lako.

Tafuta michezo ya kuigiza kwenye kituo chetu cha YouTube:

*www.youtube.com/c/Childrenareimportant*

## Kadibodi ya Silaha na Ubunifu Rahisi wa Mandhari

Kwa michezo yetu ya kuigiza, tunatumia masanduku ya kadibodi, riboni, na kung'uto/vikaangio ili kutengeneza vipande vya silaha visivyokuwa na gharama kubwa. Pata maagizo kuhusu jinsi ya kutengeneza koti ya silaha ya puto ndefu na mawazo mengine katika sehemu ya mawazo ya ziada.





### Helmet of Salvation

Strainer or pan

Ribbon

Towel to make it softer on the head





## KINGA YA KIFUANI YA HAKI

Sanduku kubwa la kadibodi
Riboni/gundi ya silikoni
Ushonaji utaimarisha katika mikunjo







## NGAO YA IMANI

Kipande cha sanduku 1 kubwa
Mfuko wazi wa plastiki
Gundi ya silikoni

## KIFAA CHA MAOMBI/MAWASILIANO

Sanduku 1 ndogo
Kipande cha waya
Ili kuweka alama katika sanduku iliyokunjwa:




## MSHIPI WA UKWELI

Kwenye mshipi wako unaweza kufunga vifaa muhimu, kama vile manati, darubini, mkanda na kantini.





## VIPANDE

Kila kipande kinahitaji kipande cha kadibodi na gundi ya silikoni/kawaida.
















### Manati



### Kamba




### Darubini




Funga upande wa chini kama sanduku la kadibodi.

## Kantini

Rejelea sehemu ya maoni ya ziada ili kuona jinsi ya kuunda kantini kwa kutumia sahani mbili za kutupwa na tyubu ya karatasi ya tishu.






Weka vipande hivi katika mshipi wa kawaida.

**UBUNIFU WA MANDHARI**

Kwa michezo 10 ya kuigiza:
Ngazi
Masanduku 2 ya kadibodi
Jedwali
Chombo cha maji
Vipande vidogo vya karatasi




## MAWAZO YA ZIADA

### MINARA MIDOGO YA PUTO




Tuunde minara au safu wima mbili kwa kutumia puto za rangi ya hudhurungi, kijani kibichi na nyeusi.
Hebu tuunde safu wima ndogo za rangi nne.
Unda jozi mbili (puto 2 zilizofungwa) na puto 1 ya kijani na 1 nyeusi na jozi nyingine ya puto 1 nyeupe na 1 hudhulungi.
Kidokezo: Kumbuka kuzifunga karibu na tumbo la puto kadiri uwezavyo ili kuzitumia vizuri.
Sasa funga jozi na uzisokote pamoja.
Rudia mchakato huu kama mara 8 zaidi ya kuwa na robo 9 za puto.
Weka robo ya kwanza katika muundo wa x ukitumia rangi ya kijani kama rejeleo. Sasa weka robo inayofuata katika muundo wa + na uiongeze kwenye robo ya kwanza kwa kutumia riboni iliyosokotwa ili kuzuia zisisonge. Endelea kuunda robo hizo zingine, na kurudia kila wakati baina ya: x, +, x, + nk.




Kidokezo: katika sehemu ya juu ya mnara wako mdogo unaweza kuweka puto ya nyota ya chuma.
Tuna video inayopatikana kwa maagizo ya jinsi ya kuunda minara ya puto ndogo.
https://youtu.be/hut9db-ALOI
Au utafute katika kituo chetu cha YouTube:
http://youtube.com/c/Childrenareimportant

### ISHARA YA MAPAMBO KWA KARATASI



Utahitaji karatasi za ukubwa wa herufu za rangi za kijani, hudhurungi, kijivu, nyeusi, mkasi, penseli, rula, na kamba.
Tutafanya muundo wa pembetatu. Weka karatasi kimlalo, kunja karatasi ya ukubwa wa herufi kwa nusu, kata karatasi na utumie nusu pekee ili kuunda muundo, kwa kutumia rula pima upana wa karatasi na uweke alama katikati. Kwa mfano, ikiwa unapima sentimita 14 weka alama katika sentimita 7. Sasa chora mstari kutoka kwa alama hiyo kwenda katika pembe ya juu kushoto na urudie hatua hii katika pembe ya juu kulia. Umbo la pembetatu litakuwa limesalia. Kata sehemu za ziada na utakuwa na muundo wako. Mara baada ya kuunda pembetatu kadhaa kwenye karatasi za rangi, unaweza kuzichanganya ili zivutie zaidi
Sasa gundisha pembetatu kwenye kamba. Usiache nafasi kati ya moja na nyingine.




### MASANDUKU YA KADIBODI

Pata masanduku ya kadibodi ya ukubwa tofauti, alama ya kudumu, karatasi ya ufundi au karatasi ya kahawia na utepe.

Funika masanduku ya kadibodi kwa kutumia karatasi. Pamba masanduku kwa kutumia mistari na maneno kama "helmeti ya wokovu" au "viatu vya injili" na upange masanduku kadhaa ili kupamba mandhari ya darasa.




### ASKARI WA PARACHUTI

Unahitaji askari wa plastiki, vichujio vya kahawa, kadibodi, utepe, na riboni/uzi. Unganisha kichujio cha kahawa na askari wa plastiki kwa kutumia riboni iliyosokotwa. Katika sehemu ya juu ya kichujio unaweza kubandika mshipi wa utepe ili kufunga katika mlango wa sebule yako au mahali ambapo unataka kupamba. Badala ya "Silaha" ya jadi, askari hawa wanashikilia maneno tofauti ambayo yanaambatana na masomo katika mpango huu: imani, ukweli, amani, wokovu, nk.



### KANTINI KWA KUTUMIA SAHANI ZA KARATASI NA TYUBU

Sahani mbili za kutupa au kadibodi mbili za mduara za takriban sentimita 10, gundi, mkasi, rangi ya hudhurungi na kijani au karatasi zilizokatwa za rangi tofauti za kijani na hudhurungi, tyubu ya karatasi ya usafi (tybu moja inatosha kwa watoto wawili) au unaweza kutumia chupa ya plastiki ya soda, na riboni iliyosokotwa.


**Maagizo**:

Chora umbo la U (herufi kubwa) lenye upana wa tyubu ya karatasi katika kila sahani, hakikisha zinalingana, na ukate zilingane.

Gundisha tyubu ya karatasi kwenye sahani ambapo imekatwa katika umbo la "U". Panga sahani hiyo nyingine katika sehemu ya juu na ugundishe pamoja.

Unaweza kupamba kwa njia mbili. Chaguo moja ni kwa kutumia rangi ya kahawia na kijani. Chaguo lingine ni kukatakata vipande vya karatasi ya kijani na hudhurungi katika rangi tofauti na kisha kuzigundisha karibu na kingo za sahani. Unda shimo ndogo kwa kila upande na ufunge riboni iliyosokotwa au uzi.

# NYENZO ZINAZOPATIKANA




### KITABU CHA MWALIMU
Masomo 10 kwa vikundi vyote vya umri

### VITABU VYA WANAFUNZI
Rahisi - miaka 4-6
Wastani - miaka 7-9
Ngumu - miaka 10-12
Ngumu zaidi - miaka 13+







### BANGO NA KIPEPERUSHI
Alika watoto zaidi!





### CHETI
Toa kwa kila mtoto mwishoni mwa programu




### ALAMA ZA CHEO/UTOFAUTI
- Mahudhurio ya darasa
- Kazi ya katikati kwa wiki kuhusu maisha
- Kazi ya kusoma: kitabu cha Matendo
- Kukariri: mafungu ya Silaha ya Mungu

### UFUNDI:
Ufundi 3 ili kusaidia katika shughuli za darasa lako







## NYIMBO ZINAZOJUMUISHA VITENDO

Wimbo halisi kwa kila moja ya masomo 10

## MICHEZO YA KUIGIZA

Mchezo mwenye utani kabisa katika kila moja ya masomo 10 (bila kuzungumza/bila lugha)






## MITANDAO YA KIJAMII

Tupate kwenye mitandao ya kijamii ili upate mawazo zaidi na msukumo kwa ajili ya huduma yako ya watoto.


YouTube facebook. WhatsApp

## TOVUTI

Pakua nyenzo hizi zote katika tovuti yetu, pamoja na nyenzo za mafunzo kwa waalimu na viongozi.



## JINSI YA KUCHAPISHA NYENZO HII:



# SOMO LA 1

## KICHWA - SOMO LA 1

Ulimwengu usioonekana

## HADITHI YA BIBLIA – SOMO LA 1

Yesu apaa mbinguni
Matendo 1:1-11

## ALAMA ZA CHEO - SOMO LA 1




Kila mtoto anapokea msingi wa alama 2 za cheo, moja kwa ajili ya kuhudhuria na nyingine kwa kusoma na kukariri.
Alama ya cheo ya mahudhurio ya leo:



Kuanzia wiki ijayo, wanafunzi wanaweza kuanza kupata zawadi kutokana na kusoma, kukariri, na kumaliza kazi ya nyumbani.

## MCHEZO WA KUIGIZA – SOMO LA 1

Askari Mcheko na Askari Zamu wanasajiliwa kujiunga na jeshi. Askari Mcheko anaamini kuwa hakuna maadui na anataka tu kuvaa mavazi yanayovutia, kuongeza nguvu, na kuonekana kama anaigiza sinema. Sajenti Mlingoti anaanza mafunzo ya kwanza ya kuandamana pamoja na hotuba kuhusu jinsi ya kupigana na adui.

## MSTARI WA KUMBUKUMBU – SOMO LA 1

"Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani." Waefeso 6:10-11

## SOMO KUU - SOMO LA 1

**Matendo 1:1-11**

Kuna ulimwengu usioonekana karibu nasi na upo kihalisia, ingawa hatuwezi kuuona. Kama tu jinsi hauwezi kuona upepo, lakini unaweza kuona jinsi miti inavyosonga wakati upepo unavuma kupitia majani, ndivyo ilivyo katika ulimwengu wa kiroho. Mmoja wa manabii wa Agano la Kale, Elisha, anatoa mfano mzuri wa kuona ulimwengu huu usioonekana. Kuna vita vinavyokaribia kuanza kati ya Aramu na Israeli. (2 Wafalme 6: 8-23) Usiku mmoja, askari wa maadui walizunguka jiji, na wakati mtumishi wa Elisha alipowaona, aliogopa sana. Lakini nabii akamwambia mtumishi wake asiogope kwani kulikuwa na askari zaidi katika upande wao kuliko upande wa adui. Ndipo Elisha akaomba ili macho ya mtumishi wake yafunguliwe, alipotazama aliona vilima vilivyojaa farasi na magari ya moto yakiwazunguka! Mungu alikuwa na jeshi kubwa lisiloonekana lililomlinda nabii wake!

Kuna vita vya kiroho vinavyotuzunguka, ingawa hatuwezi kuviona. Bibilia inaweka wazi kuwa Shetani yuko na anajaribu kutufanya tupuuze ukweli wa ufalme wa kiroho. Katika hadithi ya leo ya Bibilia kutoka kitabu cha Matendo, tunaona Yesu akipaa mbinguni. Tafadhali niamini, mbingu na kuzimu zipo. Katika hadithi hii ya kihistoria, baada ya Yesu kupaa, malaika wawili walijitokeza kwa wanafunzi! Ni vigumu kuwaza malaika wakija ili kutusaidia au shetani akitushambulia, lakini vitu hivi vipo kihalisia. Wacha tuangazie somo hili kuhusu Silaha

ya Mungu na tujifunze zaidi kuhusu ulimwengu huu usioonekana. Tuko kwenye vita, iwe tunaitikia au tunapuuza.Kwa hivyo, hebu tuvalie Silaha kamili ya Mungu tunapopigana na adui!

## KAMBI YA MAZOEZI - SOMO LA 1



### KAZI YA ZIADA – SOMO LA 1

Chora picha yako pamoja na malaika anayekusaidia kwa njia fulani. Waza kuhusu hali kadhaa hatari na za kutisha ambazo zinakukabili.

### KAZI YA NYUMBANI (WANAFUNZI WAKUBWA) - SOMO LA 1

Soma Matendo 1-4

## POWERPOINT / UAMUZI - SOMO LA 1

"Ninachagua kuamini katika ulimwengu huu usioonekana na kuvaa Silaha kamili ya Mungu."

## MASWALI NA MAJIBU - SOMO LA 1

1. Je, una ushahidi wowote kuhusu ulimwengu usioonekana wa mema na mabaya?
Wahimize wanafunzi wako wasimulie hadithi za watu ambao walikuwa karibu kuumia kutokana na ajali au ugonjwa lakini walinusurika bila majeraha ya kudumu. Ndoto na "maono juu ya kitu" wakati mwingine hutuongoza ili kufanya chaguo bora ambazo zinaonekana kama zinawezekana bila msaada wa nje. Wakati mwingine hofu hutuathiri, na tunaweza kumwambia Shetani atuache na kuhisi amani ndani mwetu.
2. Je, umeshuhudia wengine ambao wametenda makosa na hawaonekani kulindwa na Silaha ya Mungu? Shiriki hadithi kadhaa.
Wazo ni kuwafanya wanafunzi washiriki hali ambazo wameshuhudia na kutambua kwamba bila Silaha ni rahisi kufanya makosa au dhambi. Usitumie majina halisi! Wahimize wanafunzi wazungumzie kuhusu mtu wanayemfahamu ambaye aliwahi kumpenda Yesu na kuhudhuria kanisa, lakini sasa hafuati Yesu.
3. Je, unadhani vita vya kiroho vinavyotuzunguka vinakaaje?
Zungumzia kuhusu mifano ya malaika na pepo wanaopatikana katika Bibilia. (Mfano: Danieli 7, 9: 21-23, 10: 5-14)
4. Je, ni nani aliyetoa ahadi kwamba Yesu atarudi kwa njia ile ile aliyoondoka?
(Wanaume wawili waliovaa mavazi Meupe, labda malaika.)
5. Jaza nafasi tupu zinazotoka katika kitabu cha Matendo 1:8: Mtakuwa mashahidi wangu katika …________________________________________. Je, maneno haya yana maana gani kwetu sasa?
(Yerusalemu, kote Yudea na Samaria hadi mwisho wa dunia. Tunahitaji kushuhudia, kuwaambia watu kuhusu Yesu kote tuendapo.)

## MCHEZO: MAPINDUZI - SOMO LA 1



### NYENZO

Karatasi, kalamu, puto, na muziki (sio lazima.)

### MAANDALIZI

Andika majina ya masomo 9 yanayofuata kwenye karatasi. Weka pumzi katika puto na uweke karatasi lililo na somo ndani ya kila puto kabla ya kuifunga.

### KUCHEZA MCHEZO

1. Wanafunzi wanaunda mduara na kupitisha puto 1 kuzunguka mduara. (Mwanafunzi wa kwanza anaipitisha juu ya kichwa, wa pili anapitisha katikati ya miguu yake, nk.) Mpaka mwalimu aseme kwa sauti au apige filimbi. (Chaguo: Cheza muziki wa kusisimua wanapopitisha puto.)
2. Wakati mwalimu anatoa sauti, mwanafunzi aliye na puto anaelekea katikati na analipua puto kwa kutumia mguu mmoja. Kisha mwanafunzi anaondoa karatasi iliyo ndani na kuisoma kwa wengine.
Wanaendelea kucheza hadi watakapomaliza puto zote.


## CHAGUO

1. Ikiwa una wanafunzi wengi, unaweza kuunda miduara kadhaa, au upitishe puto zaidi ya moja kwa wakati mmoja.
2. Pamoja na karatasi zilizo na vichwa, unaweza pia kuweka pipi au maagizo tofauti katika puto (kama vile kukimbia na kuzunguka kanisa mara moja, nk.)

## MAJIBU YA FUMBO - SOMO LA 1

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| N | I | T | U | N | E | R | O | H | O | Y |
| M | A | J | I | M | A | F | N | G | M | U |
| H | M | L | L | G | W | U | U | K | I | S |
| I | B | A | I | R | Z | N | M | U | T | F |
| N | F | F | S | O | I | D | B | W | U | A |
| U | W | G | Z | H | T | I | A | B | M | L |
| G | U | M | E | L | [illegible] | S | U | R | E | Y |
| N | S | V | W | H | B | H | M | S | Z | K |
| I | H | B | U | Y | U | A | I | A | E | U |
| B | I | Z | A | G | K | J | B | D | J | Y |
| M | D | I | W | I | N | G | U | A | I | F |





# SOMO LA 2

## KICHWA - SOMO LA 2
Pambana na giza

## HADITHI YA BIBLIA – SOMO LA 2
Paulo na Sila gerezani
Matendo 16:16-31

## ALAMA ZA CHEO - SOMO LA 2




Alama za Cheo za Mahudhurio ya leo:
Kila mwanafunzi aliyeshiriki katika "kambi ya mazoezi" ya wiki iliyopita anapokea "riboni" hii:



Kila mwanafunzi aliyemaliza shughuli ya kusoma kwa wiki iliyopita kutoka kwa kitabu cha Matendo anapokea nyota.

Kila mwanafunzi anayeweza kukariri mstari wa kumbukumbu wa wiki iliyopita anapokea nyota.

## MCHEZO WA KUIGIZA – SOMO LA 2
Askari Zamu na Mcheko wanaingia huku wakibishana baina yao. Sajenti Mlingoti anawafanya Askari Mcheko na Zamu wapitie kozi ya vikwazo, na wao wanabishana wakati wote wa kozi. Baada ya kumaliza kozi ya vikwazo, askari wanapigana tena. Sajenti anasimamisha mapigano, akiwaambia kwamba vita havifai kuwa baina yao lakini dhidi ya adui.

## MSTARI WA KUMBUKUMBU – SOMO LA 2
"Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho."Waefeso 6:12


## SOMO KUU - SOMO LA 2
**Matendo 16:16-31**

Hatupigani na wanadamu lakini tunapingana na shetani na ukuu wake wa giza. Shetani anapenda kusababisha kutokuelewana na anaweza kutumia watu kuumiza wengine, lakini lazima tukumbuke kila wakati kuwa vita vyetu ni dhidi yake! Ulimwengu wetu ni mahali palipojaa dhambi, na kama wanadamu, mara nyingi tunatenda dhambi dhidi ya wenzetu. Lakini lazima tukumbuke kutopigana dhidi yetu, kwa sababu tunapofanya hivyo tunakuwa tumeanguka katika mtego wa adui.
Mungu anapenda kila mtu, hata ingawa tunafanya makosa. Tunashukuru Mungu kwa huruma zake tunapofanya makosa, kwa hivyo tunapaswa pia kuwahurumia wengine. Wakati mwingine adui anapotosha maneno au matendo yetu, ili tukasirike zaidi. Walakini, Mungu anapenda kila mtu, na hivyo tunapaswa kupenda kila mtu.
Katika hadithi ya leo ya Bibilia kutoka kitabu cha Matendo, Paulo na Sila wanafungwa gerezani. Walinzi wanawatendea mabaya, ingawa hawajafanya chochote kibaya. Walakini, Mungu anapowapa njia ya kutoroka, hawalipizi kisasi kwa walinzi, badala yake wanawaonea huruma, na kumwongoza mlinzi na familia yake yote

kukubali Bwana katika maisha yao! Paulo na Sila wangemlaumu mlinzi kwa uovu dhidi yao, lakini badala yake walikumbuka kwamba vita vyao vilikuwa dhidi ya shetani na sio dhidi ya walinzi. Lazima tukumbuke tunapovaa Silaha ya Mungu, kupigana na giza ya kiroho na sio dhidi ya wanadamu wenzetu!

## KAMBI YA MAZOEZI - SOMO LA 2

### KAZI YA ZIADA – SOMO LA 2



Kuwa macho kwa vitendo na maneno ya watu walio karibu nawe na utambue shambulio la kiroho. Unaposhuhudia au kusikia mtu akimdhulumu mtu mwingine, tambua kuwa Shetani anafurahia kitendo hicho na jinsi Mungu anavyohuzunishwa na kitendo hicho. Jitayarishe kumwelezea mwalimu wako kile kilichotendeka, bila kutaja majina.

### KAZI YA NYUMBANI (WANAFUNZI WAKUBWA) - SOMO LA 2

Soma Matendo 5-7

## POWERPOINT / UAMUZI - SOMO LA 2


"Nachagua kupigana na adui, na sio watu walio karibu nami."

## MASWALI NA MAJIBU - SOMO LA 2

1. Je, maneno haya yana maana gani? "nguvu, mamlaka, na nguvu, ambazo zinatawala ulimwengu huu wa giza na pepo mbaya za kiroho." Waefeso 6:12
Wazo ni kufanya wanafunzi watambue kuwa wamo katika vita, na kwamba shetani na pepo wake wote wapo, hata kama hatuwaoni. I Petro 5:8; Ufunuo 12:9
2. Je, ni mifano mingine ipi ambapo tumepigana na wanadamu badala ya ulimwengu wa giza?
Mfano: wakati mtu anakuchekelea unaposoma au kuhubiri Neno. Tunapokuwa na tabia ya unyenyekevu, lakini watu wanafikiria sisi ni wajinga. Ruhusu wanafunzi watoe mifano.
3. Je, kwa nini Mungu alitaka tufahamu kuhusu Silaha ya Mungu?
Anataka tufahamu kuwa yuko pamoja nasi kila wakati na hatarajii tuwe na nguvu za kusimama imara katika ulimwengu tukiwa peke yetu Anatuandaa na silaha ambazo tunahitaji ili kusimama dhidi ya shetani. Anatuambia kwamba "Vaa Silaha" kwa sababu tunaweza kuchagua kukataa msaada Wake na kujaribu kufanya mambo kulingana na nguvu zetu wenyewe.
4. Je, ni kitu gani kilichokuwa na uchungu kiliwatendekea Paulo na Sila kabla ya kutupwa gerezani? Walipigwa hadharani kwa vijiti. Matendo 16:22-23,37
5. Je, jibu kwa swali la mlinzi wa gereza, "Nifanye nini ili niokolewe?" lilikuwa gani?
Walimwambia, "Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka, wewe pamoja na jamaa yako." Matendo 16:31

## MCHEZO: VITA - SOMO LA 2

### NYENZO



Mpira mdogo wa uzi kwa kila kikundi cha wanafunzi 6.

### KUCHEZA MCHEZO


1. Eleza wanafunzi waunde vikundi vya wanafunzi 4-6 na kuwaweka katika safu, na kuacha nafasi kubwa kati ya kikundi kimoja na kingine.
2. Jadili na wanafunzi kwamba wakati mwingine shetani hutumia watu kutufunga, lakini kwa hali yoyote, ni shetani tunayepambana naye. Katika mchezo huu, sisi ndio tunajifunga, lakini ili tujikomboe, tunapaswa kuondoa uzi na kuwa waangalifu ili tusipigane na wengine
3. Mpe mwanafunzi wa kwanza mpira mdogo wa uzi. Mwanafunzi wa kwanza anashika ncha ya uzi na anapitisha mpira kupitia safu hadi ufike mwisho, mwanafunzi wa mwisho anaupitisha nyuma ya mgongo wake na anaupitisha kurudi mwanzoni.
4. Baada ya timu kumaliza uzi wa mipira yao, kazi yao ni kutoroka mitego ya adui, na kujikomboa kutoka kwa uzi. Timu ya kwanza kujiondoa inakuwa washindi.

### CHAGUO


Unaweza kutoa tuzo au makofi kwa kikundi kinachoweza kujiondoa bila kupigana kati yao.

## MAJIBU YA FUMBO - SOMO LA 2

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| W | A | F | U | N | G | W | A | S | K | I |
| U | A | P | A | U | L | O | J | O | I | T |
| M | T | T | V | F | W | K | R | G | M | I |
| T | U | V | U | W | J | O | K | N | B | U |
| U | M | M | A | M | R | V | U | A | A | S |
| M | Z | J | A | O | I | U | S | L | I | A |
| W | H | E | Y | T | F | S | I | I | B | L |
| A | G | N | H | S | I | S | H | M | F | A |
| B | I | O | K | I | B | M | O | I | N | M |
| M | A | L | E | J | I | T | A | K | S | A |





# SOMO LA 3

## KICHWA - SOMO LA 3
Kuwa na Msimamo

## HADITHI YA BIBLIA – SOMO LA 3
Kifo cha Stefano
Matendo 6:8-15, 7:51-60

## ALAMA ZA CHEO - SOMO LA 3
Alama za Cheo za Mahudhurio ya leo:
Kila mwanafunzi aliyeshiriki katika "kambi ya mazoezi" ya wiki iliyopita anapokea "riboni" hii:




Kila mwanafunzi aliyemaliza shughuli ya kusoma kwa wiki iliyopita kutoka kwa kitabu cha Matendo anapokea nyota.

Kila mwanafunzi anayeweza kukariri mstari wa kumbukumbu wa wiki iliyopita anapokea nyota.

## MCHEZO WA KUIGIZA – SOMO LA 3
Sagenti Mlingoti anaamrisha Askari Mcheko na Zamu wasalie kama wamesimama wakiwa makini. Kisha, Sajenti Mlingoti anapiga kelele kubwa nyuma ya askari hao. Wanaruka na kutoroka. Mara ya pili wanaogopa, wanaruka juu ya mwingine. Mara ya tatu Sajenti anatumia vikaangio ili kutoa kelele kubwa. Mwishowe, askari kwa kutumia maagizo ya Sajenti wanasimama kidete.

## MSTARI WA KUMBUKUMBU – SOMO LA 3
"Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama." Waefeso 6:13

## SOMO KUU - SOMO LA 3
**Matendo 6:8-15, 7:51-60**

Tunapojifunza kuhusu Silaha ya Mungu na kitabu cha Matendo, ni muhimu kutambua kwamba tunaweka Silaha ya Mungu na kuitumia. Hauwezi kuomba ili uweze kuvaa mshipi wako wa ukweli. Unaposema ukweli kupitia kinywa wako, na kuamini ukweli wa Mungu moyoni mwako, hapo ndipo unapovaa mshipi wa ukweli. Wala hauwezi kuomba ili kuchukua ngao yako ya imani. Unapoishi na imani, ukiamini kile Mungu anasema na sio kile wanachosema watu, basi inamaanisha umechukua ngao yako ya imani mikononi mwako na unaitumia kujilinda dhidi ya adui. Na vile vile unatumia kanuni hii ili kuwa na msimamo. Hauwezi kuomba vifungu fulani ili kuwa na msimamo. Unapomwamini Mungu na kukataa kukata tamaa, unapata msimamo.
Stefano ni mfano mzuri kwetu katika hadithi ya leo ya Bibilia kutoka kitabu cha Matendo. Alikuwa mtu mwadilifu na mwenye busara, ambaye alivaa Silaha yake kila wakati. Wakati upinzani wa kidini ulipomkabili, alisimama kidete na kile alichoamini, ingawa ilimaanisha kifo chake.

Viongozi wa dini walimkasirikia sana kwa kuhubiri kuhusu Yesu Kristo hivi kwamba walichochea umati wa watu ili watoe vurugu na mwishowe wakampiga Stefano kwa mawe. Katika hadithi hii yote ya Bibilia, Stefano alisimama kidete na kile alichokiamini, na hakubadilisha maoni yake kulingana na maoni ya umma. Kama unaamini Mungu wako na upo tayari kuteswa kwa ajili ya hilo, simama wima, na usimame imara kama umevaa Silaha kamili ya Mungu!

## KAMBI YA MAZOEZI - SOMO LA 3



### KAZI YA ZIADA – SOMO LA 3

Leta Bibilia shuleni na usifiche kwenye mkoba au mfuko wako.  Kuwa na msimamo kwa kile unachokiamini na usione aibu kuwa Mkristo.


### KAZI YA NYUMBANI (WANAFUNZI WAKUBWA) - SOMO LA 3

Soma Matendo 8-10

## POWERPOINT / UAMUZI - SOMO LA 3

"Nachagua kusimama kidete."

## MASWALI NA MAJIBU - SOMO LA 3



1. Je, maisha ya mwanadamu yana mazuri na mabaya gani?
Mfano: Mwanafunzi katika muhula mmoja anapata alama nzuri na muhula unaofuata anapata alama mbaya sana. Mtu ambaye siku moja ana furaha nyingi lakini muda unaofuata amejawa na masikitiko. Mtu ambaye ana pesa nyingi lakini anapoteza zote na kuwa maskini. Mtu ambaye anasema ana nguvu na hana dhambi, lakini anapatikana akijihusisha na dhambi ya ngono.
2. Je, ni lini tunahitaji kusimama dhidi ya Shetani?
Tunapojaribiwa kusema uwongo. Wakati mtu anatuhimiza tuingie mahali ambapo watoto hawapaswi kuingia, au tunapokuwa karibu kuiba kalamu inayotupendeza sana.Lazima tuwe wenye msimamo kwa sababu tuko kwenye vita vya kila wakati.
3. Je, ni kitendo gani muhimu zaidi tunahitaji kufanya ili tuweze kusimama kidete?
Jifunze kuishi kwa njia ambayo kila wakati tumevaa Silaha zetu.
4. Je, ni nani anayejulikana kuwa na uso kama wa malaika wakati anashtumiwa kwa uwongo?
Stefano
5. Je, alisema nini kabla ya kufa kwake?
"Bwana, usiwalaumu kwa dhambi hii." Matendo 7:56 na Matendo 7:59-60

## MCHEZO: VITA - SOMO LA 3

### NYENZO

Mpira, utepe wa kufunga

### MAANDALIZI

Weka alama katika nafasi za wachezaji kwenye sakafu au ardhi.

### KUCHEZA MCHEZO


1. Gawanya darasa lako katika vikundi viwili, ikiwa una wanafunzi zaidi ya 20 tunapendekeza kucheza kwa zamu za wachezaji wasiozidi 8 kwa kila timu.
2. Wacheza wanawekwa kwenye alama ambazo zimewekwa kwenye sakafu au ardhini na zilizowekwa kwa umbali wa mkono mmoja.
3. Mwalimu anatupa mpira kwa upole. Timu moja inajaribu kuweka mpira katika upande mmoja wa goli, na timu nyingine inaweka katika goli hilo lingine.
4. Wacheza hawawezi kusonga kutoka kwa mahali pao na wanaweza kuzunguka tu, wakisogeza mguu mmoja kwa wakati hadi watakapofunga.

**CHAGUO**


1. Unaweza kucheza kwenye sakafu na kuweka alama kwa kutumia utepe wa rangi.
2. Wachezaji wanaweza kuketi kwenye viti badala ya kusimama.

## MAJIBU YA FUMBO - SOMO LA 3

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | T | E | F | A | N | O | E | F | M | W |
| M | B | I | N | G | U | N | R | U | A | C |
| A | G | N | A | H | C | M | O | S | J | H |
| D | B | A | N | A | W | B | H | E | O | A |
| S | H | J | F | A | G | I | O | Y | H | N |
| A | T | A | N | J | T | N | W | A | O | G |
| E | W | A | M | A | W | G | I | P | U | K |
| T | Y | H | K | B | M | U | O | J | O | A |
| E | E | I | G | Y | I | N | T | E | I | T |
| T | S | A | B | M | O | I | L | A | G | M |







# SOMO LA 4

## KICHWA - SOMO LA 4
Mshipi wa Ukweli

## HADITHI YA BIBLIA – SOMO LA 4
Anania na Safira
Matendo 5:1-10

## ALAMA ZA CHEO - SOMO LA 4

Alama za Cheo za Mahudhurio ya leo:
Kila mwanafunzi aliyeshiriki katika "kambi ya mazoezi" ya wiki iliyopita anapokea "riboni" hii:




Kila mwanafunzi aliyemaliza shughuli ya kusoma kwa wiki iliyopita kutoka kwa kitabu cha Matendo anapokea nyota.

Kila mwanafunzi anayeweza kukariri mstari wa kumbukumbu wa wiki iliyopita anapokea nyota.




## MCHEZO WA KUIGIZA – SOMO LA 4
Askari Mcheko anajivuna kuhusu kitu kisicho cha kweli kwa Askari Zamu wakiwa katika kambi, kisha anaacha mshipi wake. Kwenye shughuli ya mafunzo, Askari Mcheko anaendelea kuomba usaidizi wa vifaa kutoka kwa Askari Zamu. Wakati Sajenti Mlingoti anapomwuliza Mcheko kuhusu mshipi wake, anasema uongo. Mwishowe, Mcheko anamwambia Sajenti ukweli kwamba aliacha mshipi wake, anaomba msamaha kwa Zamu kwa kumwambia uongo, na anarudi ili kuchukua mshipi wake.

## MSTARI WA KUMBUKUMBU – SOMO LA 4
"Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani" Waefeso 6: 14a"

## SOMO KUU - SOMO LA 4
**Matendo 5:1-10**

Sehemu ya kwanza ya Silaha iliyotajwa katika Waefeso sura ya 6 ni mshipi wa ukweli, kifaa ambacho kinafungwa kiunoni na askari na kusaidia kushikilia pamoja Silaha nzima. Mshipi unashikilia Silaha katika mwili wa askari, unashikilia upanga mahali pake, na ni kifaa ambacho askari hawezi kuondoa. Kwa kweli, ikiwa askari hana mshipi wa ukweli, labda hata mavazi yake yataanguka chini, na kuaibika mbele ya kila mtu!
Sehemu moja ya ukweli ni mambo tunayosema na vinywa vyetu. Tunapaswa kuwa Wakristo ambao husema ukweli tu, sio kusema uwongo kwa wazazi wetu au kwa Mungu. Lakini sehemu nyingine ya mshipi wa ukweli ni kwamba tunachagua kumwamini Mungu na Neno Lake. Ukweli ni kwamba adui yetu, Ibilisi, kila wakati anajaribu kusema uwongo na kutudanganya kwa kuamini vitu ambavyo sio vya kweli.
Katika hadithi ya leo ya Bibilia, Anania na Safira waliamini uwongo kwamba haikuwa muhimu kuwa waaminifu mbele ya wanafunzi. Walijifanya kuwa wameuza mali zao kwa pesa kidogo kuliko zile walizopata. Waliamini adui ambaye aliwafanya wadhani kwamba Mungu hangewaona au hakujua maelezo ya mauzo. Lakini Mungu

huona kila kitu. Wanafunzi walikuwa wawakilishi tu wa Mungu. Na kwa sababu walisema uwongo mbele ya wanafunzi, hivyo walisema uwongo mbele ya Mungu. Walificha ukweli kuhusu mauzo yao kwa sababu waliamini uwongo ambao shetani aliwafanya waamini. Je, ni uongo gani unaoamini ambao unaweza kusababisha Silaha yako ianguke? Ni muhimu kwamba kila wakati tuvae mshipi wa ukweli kwa kusema ukweli kila wakati na kwa kuamini ukweli kuhusu Mungu na Neno lake kila wakati.

## KAMBI YA MAZOEZI - SOMO LA 4

### KAZI YA ZIADA – SOMO LA 4



Fikiria kuhusu uwongo uliyosema hapo mbeleni na uandike. Hata kama haukufanyika hivi majuzi, wakati ukiwa mdogo. Sasa orodhesha uwongo wote uliofuata ili kufanya uwongo wa kwanza usigunduliwe. Andika watu walioathirika kwa sababu ya uwongo huo?

### KAZI YA NYUMBANI (WANAFUNZI WAKUBWA) - SOMO LA 4

Soma Matendo 11-13

## POWERPOINT / UAMUZI - SOMO LA 4

"Nachagua kuishi kwa uaminifu."

## MASWALI NA MAJIBU - SOMO LA 4

1. Ikiwa wewe sio mwaminifu, nini kinafanyikia mshipi wako wa kweli? Je, hili litaathiri sehemu zingine za Silaha yako?

Tunakosa kuvaa mshipi wa ukweli wakati tunasema uwongo au tunapokosa uaminifu, na kuishi kwa njia hii kutaathiri vibaya maisha yetu yote.Mshipi unashikilia suruali yako au sehemu zingine za Silaha yako. Bila uaminifu, watu hawawezi kutuamini tena.

2. Je, ni hali gani ambapo husemi 'uongo' lakini unakosa 'uaminifu'?

Ruhusu wanafunzi wafikirie kuhusu hali kama hiyo. Mfano: Unaenda shule lakini hasomi au hufanyi kazi uliyopewa. Unawaambia wazazi wako kuwa mlikuwa na marafiki zako lakini huwaambii mlichokuwa mkifanya. Au, unapata alama nzuri katika mtihani lakini hausemi kwamba ulinakili majibu kutoka kwa rafiki.

3. Matokeo ya uwongo ni gani?

Unaathiri uaminifu. Mfano: unadanganya mama yako, anapogundua kwamba ulisema uongo hatoweza kuamini chochote unachosema kuwa cha kweli kwa muda mrefu. Matokeo mengine ni kwamba lazima ujitahidi kukumbuka uwongo na kubuni "hadithi" hiyo hiyo kila wakati. Jambo hilo sio rahisi. Ikiwa utakosea mara moja, unajulikana kama mwongo.

4. Anania na Safira wote waliwezaje kusimulia hadithi inayolingana kuhusu mauzo ya mali zao ingawa kulikuwa na muda wa saa tatu walipongumza na Petro

Hadithi ilikuwa uwongo uliopangwa: iliyoandaliwa mapema. Matendo 5:2, 9

5. Anania na Safira walimwambia nani uwongo? Watu wanaposema uwongo leo, wanamdanganya nani

Walifikiria wanadnaganya Petro, lakini ilikuwa Mungu.

Matendo 5:4

## MCHEZO: VITA - SOMO LA 4

### NYENZO

Filimbi

### KUCHEZA MCHEZO



Wanafunzi wanasimama katika safu wakiangalia mbele. (Na kuacha nafasi ya umbali kati ya mwalimu na wanafunzi ya angalau mita 12) Mwalimu anageuka upande huo mwingine na kusema kwa sauti "kimbia." Watoto wanakimbilia kwa mwalimu. Mwalimu anasema kwa sauti "Ganda" na watoto wanapaswa kusimama kama

wamegandishwa. Sema kwa sauti "zunguka" na watoto wanapaswa kugeuka... kisha "kimbia" na wanapaswa kukimbia wakielekea upande huo mwingine. Endelea kusema mambo tofauti (kimbia polepole, ruka, nk.). Mwanafunzi wa kwanza anapofikia mwalimu, anakuwa mtangazaji, na mchezo unaweza kuanza tena.

### CHAGUO

1. Piga filimbi kabla ya kusema maagizo, ili watoto wasikilize yanayofuata (hivyo hutapaswa kusema kwa sauti ya juu).
2. Ikiwa hauna nafasi kubwa, watoto wanaweza kutembea badala ya kukimbia.

## MAJIBU YA FUMBO - SOMO LA 4

Andika ukweli 5 wa Mungu katika maisha yako.

Mawazo:
Mungu ananijali.
Mungu ananipa nguvu.
Mungu ndiye msaidizi wangu.
Mungu hutimiza ahadi Zake.
Mungu yuko nami katika hali zote maishani mwangu.


| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | N | A | R | H | O | P | F | I | W | W |
| M | U | S | G | Y | U | M | W | A | E | O |
| A | G | P | O | U | W | O | N | G | O | N |
| L | N | M | E | K | E | A | S | E | P | G |
| I | U | A | O | P | U | G | A | M | | O |
| B | M | I | N | M | E | Z | F | I | H | M |
| I | U | K | E | I | G | T | I | O | V | B |
| B | V | O | E | T | A | P | R | K | U | A |
| L | U | N | G | U | V | U | A | O | W | I |
| I | K | U | O | M | B | A | P | E | T | A |
| A | S | A | F | E | R | A | W | A | N | A |

---

Andika mifano 5 ambapo unaweza kuvaa mshipi wa ukweli katika maisha yako.

Mawazo:
Wakati rafiki yangu anafanya jambo mbaya na ninafahamu hilo.
Kusema ukweli kwa walimu wangu.
Wanaponiuliza ikiwa nilidanganya katika mtihani.
Kukosa kutia chumzi kwenye hadithi.
Ninapofanya vibaya, kukubali hatia yangu.





# SOMO LA 5

## KICHWA - SOMO LA 5

Kinga ya kifuani ya haki

## HADITHI YA BIBLIA – SOMO LA 5

Kornelio
Matendo 10:9-23

## ALAMA ZA CHEO - SOMO LA 5

Alama za Cheo za Mahudhurio ya leo:
Kila mwanafunzi aliyeshiriki katika "kambi ya mazoezi" ya wiki iliyopita anapokea "riboni" hii:




Kila mwanafunzi aliyemaliza shughuli ya kusoma kwa wiki iliyopita kutoka kwa kitabu cha Matendo anapokea nyota.

Kila mwanafunzi anayeweza kukariri mstari wa kumbukumbu wa wiki iliyopita anapokea nyota.




## MCHEZO WA KUIGIZA – SOMO LA 5

Askari Mcheko na Zamu wamepokea koti zao zilizoundwa kwa kinga za changarawe. Askari Mcheko anaanza mchezo na Askari Zamu ambapo wanagongana katika koti. Wakati wa mazoezi, Sajenti Mlingoti anawapa "changarawe" laini na anagawanya katika timu. Mcheko amesahau koti lake. Wakati mafunzo yanaanza, anaendelea kugongwa na changarawe laini

## MSTARI WA KUMBUKUMBU – SOMO LA 5

"Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani"

Waefeso 6:14b


## SOMO KUU - SOMO LA 5

**Matendo 10:9-23**

Kipande kinachofuata cha Silaha ya Mungu kutoka kwa sura ya 6 ya Waefeso ni kinga ya kifuani ya haki. Haki ni kuonyesha tabia ya umungu, au kufanya kilicho sawa, kizuri na aminifu. Kitendo cha kuendelea kufanya haki mbele za Bwana ndicho kinachotunza kinga ya kifuani. Mungu anatuomba katika maandiko tuwe wenye busara na kufanya jambo sahihi. Tunapofanya hivyo, tunaweza kuwa na hakika kwamba tumevaa kinga ya kifuani, na kwamba mioyo yetu imelindwa kikamilifu wakati tuko vitani. Kuna jambo la muhimu sana kuhusu kinga ya kifuani, inafunika mioyo yetu ambayo ni chombo muhimu, lakini katika upande wa mbele tu. Tunapoivaa, tunaweza kujeruhiwa lakini bado tunaweza kuamka na kuendelea na vita. Walakini, tunahitaji kukambiliana na vita moja kwa moja kwa sababu kinga ya kifuani hufunika upande wa mbele. Haitaweza kutulinda ikiwa tumegeuka, tunapokimbia na kutoroka.
Je, tabia ya uungu na haki ni nini? Je, tunajuaje kama tunayo? Bibilia inasema kwamba Kornelio alikuwa mcha Mungu na aliyemwogopa Mungu na ambaye alitoa kwa ukarimu na alisali mara kwa mara. Bibilia pia inasema kwamba Wayahudi wote walimheshimu. Wengine watajua wakati wewe ni mwenye haki, kwa sababu kwa

wakati inakuwa dhahiri kuona. Kornelio alikuwa amevaa kinga yake ya kifuani. Wakati huo, ilikuwa kinyume cha sheria kwa Wayahudi kushirikiana na watu wa mataifa mengine au hata kuwatembelea. (Matendo 10:28) Mungu alituma maono kwa Petro ili aende kushiriki Injili na Kornelio. Kwa sababu Kornelio alikuwa mcha Mungu, Mungu alituma mtu kwake (hata dhidi ya sheria) ili kumwokoa yeye na familia yake yote!

## KAMBI YA MAZOEZI - SOMO LA 5



### KAZI YA ZIADA – SOMO LA 5

Je, ni nani unayemjua na kumheshimu kwa sababu ya jinsi anavyoishi na kuwatendea wengine? (Kama Kornelio katika hadithi ya leo ya Bibilia.) Andika sentensi inayoelezea ushahidi mmoja kuhusu maisha yao mazuri, halafu nenda uwaeleze mwenyewe kuhusu jambo hilo.

### KAZI YA NYUMBANI (WANAFUNZI WAKUBWA) - SOMO LA 5

Soma Matendo 14-16


## POWERPOINT / UAMUZI - SOMO LA 5

"Nachagua kila wakati kufanya jambo sahihi."

## MASWALI NA MAJIBU - SOMO LA 5

1. Je, ni katika hali gani za maisha yako ambapo umedhihirisha kwamba umevaa kinga ya kifuani ya haki na ni hali gani ambapo umeshindwa kuionyesha?
NDIYO: Unasaidia mzee kuvuka barabara. Kusaidia mama yako kusafisha nyumba mara kwa mara. Shiriki vitu vyako na kaka yako mdogo. HAPANA: Kuchokoza watoto wadogo shuleni. Kumchekelea kaka yako. Kumfanya mwanafunzi mwenzako afanye vibaya kwenye mtihani.
2. Fafanua jinsi unaweza danganya kuwa mwenye haki.
Bila kutumia majina halisi, eleza familia ambayo inaonekana nzuri wanapokuja kanisani. Lakini nyumbani wanakasirikiana na kupigana baina yao. Wanajivunia jinsi wanavyoweza kumwimbia mtu fedha. Wanasema utani mbaya au kuapa kwa jina la Bwana.
3. Je, ni katika hali gani ambapo unaweza kuchagua kutofanya chochote badala ya kufanya kitu kisha uaibike?
Unaweza kuchagua kutohimiza mtu ambaye sio maarufu hata kama anahitaji usaidizi. Unakosa kuombea mtu kwa sababu wanafunzi wengine wako karibu.
4. Je, Petro alienda kutembelea nyumba ya nani? Kwa nini hatua hio ilikuwa sio kawaida?
Mungu alimtuma kwenda kumuona Kornelio. Hakuwa Myahudi, na kwa kawaida Wayahudi hawakuchanganyika na wengine.
5. Je, ni kwa njia gani Kornelio alikuwa tofauti na wanaume wengine katika eneo hilo?
Kornelio alikuwa mkarimu ingawa alikuwa afisa wa jeshi. Aliitunza familia yake vizuri. Alimheshimu Mungu kwa kuwasaidia Wayahudi katika eneo lake.

## MCHEZO: ULINZI - SOMO LA 5



### NYENZO

Utepe wa kufunga, kikombe cha kutupa kwa kila mwanafunzi, mipira 1-2

### MAANDALIZI

Gawanya uwanja wa kucheza kwa mstari wa utepe.

### KUCHEZA MCHEZO


1. Gawanya darasa lako katika vikundi viwili na uweke kila kikundi katika upande tofauti wa utepe. Toa kikombe kwa kila mwanafunzi. Na wanachagua mahali pa kuweka kikombe chao karibu nao. (Isiwe zaidi ya mita 6 kutoka kwa mstari) Kisha wanafunzi wanasimama kati ya mstari na kikombe chao.
2. Toa mpira kwa moja ya timu. Mshiriki wa timu hiyo anabiringisha mpira hadi upande huo mwingine wa mstari na kujaribu kugonga vikombe vya timu nyingine wakati washiriki wengine wanalinda vikombe vyao kwa mikono na miguu yao. Mwanafunzi ambaye atashika mpira, anaubiringisha upande huo mwingine. Kila wakati kikombe kinaangushwa na mpira, mwenye kikombe anaondoka katika mchezo pamoja na kikombe

chake. Ikiwa hakuna kikombe kinachoanguka baada ya dakika chache za kucheza, ongeza mpira mwingine ili kuwe na mipira miwili kwa wakati mmoja. Maliza mchezo baada ya dakika 5, kisha wanafunzi waanze tena.

**CHAGUO**

Unaweza kutumia vikombe zaidi kuliko wanafunzi ili iwahitaji walinde zaidi ya kikombe kimoja.

## MAJIBU YA FUMBO - SOMO LA 5




| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| N | M | K | H | W | B | A | G | N | O | M |
| K | W | A | N | A | U | M | E | H | M | B |
| S | O | O | O | Y | P | O | O | M | B | A |
| I | N | R | I | N | U | R | P | W | I | N |
| M | Y | T | N | P | O | M | E | O | N | I |
| O | U | E | O | E | W | A | B | G | G | B |
| N | M | P | M | Y | L | S | L | A | U | K |
| H | A | K | I | M | B | I | Y | L | N | W |
| I | B | A | S | F | A | F | O | U | I | I |
| W | M | W | O | N | G | A | S | K | L | F |

# SOMO LA 6

## KICHWA - SOMO LA 6
Viatu vya injili ya Amani

## HADITHI YA BIBLIA – SOMO LA 6
Filipo na Mhabeshi
Matendo 8:26-40

## ALAMA ZA CHEO - SOMO LA 6




Alama za Cheo za Mahudhurio ya leo:
Kila mwanafunzi aliyeshiriki katika "kambi ya mazoezi" ya wiki iliyopita anapokea "riboni" hii:




Kila mwanafunzi aliyemaliza shughuli ya kusoma kwa wiki iliyopita kutoka kwa kitabu cha Matendo anapokea nyota.

Kila mwanafunzi anayeweza kukariri mstari wa kumbukumbu wa wiki iliyopita anapokea nyota.

## MCHEZO WA KUIGIZA – SOMO LA 6
Leo Askari Mcheko analalamika na ana wasiwasi kuhusu kila kitu. Askari Mcheko amesahau viatu vyake vya kupigana na miguu yake inaendelea kuumia wakati wa mazoezi, na kumfanya alalamike na awe wasiwasi hata zaidi. Sajenti Mlingoti anamkumbusha Askari Mcheko kwamba Jenerali Yesu anawajali na anamwagiza aache kulalamika na aende achukue viatu vyake.

## MSTARI WA KUMBUKUMBU – SOMO LA 6
"na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani" Waefeso 6:15

## SOMO KUU - SOMO LA 6
**Matendo 8:26-40**

Sasa ni wakati wa kuvaa viatu vyetu ili tuwe tayari kupiha hatua! Hii inamaanisha kwamba tuko tayari kushiriki injili, au tuko tayari kutii wakati wowote, au tuko tayari KWENDA kufanya jambo sahihi.
Kile tunachovaa katika miguu yetu huamua udhabiti na uwezo wetu wa kusonga. Viatu vinaathiri jinsi tunaweza kutembea au kukimbia. Viatu vibaya vinaweza kuathiri uwezo wetu, kupunguza kasi yetu, na kutufanya tuondoke katika mstari wa mapigano. Askari asiye na viatu anaweza kujiingiza katika hatari kubwa. Hatupaswi kuwa na wasiwasi wa mahali tunapoenda katika vita kwa sababu ya viatu vyetu. Viatu hutuwezesha tupige hatua bila uoga huku tukizingatia kamili vita vilivyo mbele yetu. Mwili wa Kristo umetumwa ili kutangaza habari njema ya Ufalme wa Mungu, ambayo itaeneza njia Yake ya amani ulimwenguni kote. Tunapovaa viatu vyetu, tunakuwa tayari kusonga, kueneza habari njema kwa wengine.
Hadithi ya Filipo kutoka kitabu cha Matendo ni hadithi nzuri inayoelezea kuhusu mtu aliye tayari kwenda kutangaza injili. Ghafla malaika anamwambia ainuke na kwenda, akimpa maelekezo fulani kuhusu barabara katika jiji. Anapofika, Bwana anamwambia akimbilie gari fulani. Filipo anamwuliza mtu huyo ikiwa anaelewa

anachosoma, anaingia kwenye gari, kisha anaendelea kushiriki injili.  Mhebeshi anaamua kumchagua Kristo na anasimamisha gari ili abatizwe papo hapo! Filipo alimbatiza, lakini walipotoka katika maji, Filipo akatoweka!  Roho wa Bwana alimpeleka Filipo mahali pengine ili aendelee kuhubiri injili.Hii ni hadithi ya ajabu sana ya mtu ambaye alikuwa tayari kwenda kuishiriki injili!

## KAMBI YA MAZOEZI - SOMO LA 6



### KAZI YA ZIADA – SOMO LA 6

Ni wakati wa kujua jinsi mtu huhisi anapokosa kuwa tayari kumwambia mtu kuhusu injili.Kwanza, fikiria ukitembea au kukimbia barabarani bila viatu vyako. Balaa! Ifuatayo, andika kile ambacho unaweza kusema kwa mtu ambaye anakuuliza umweleze jinsi ya kuwa Mkristo.

### KAZI YA NYUMBANI (WANAFUNZI WAKUBWA) - SOMO LA 6

Soma Matendo 17-19

## POWERPOINT / UAMUZI - SOMO LA 6

"Ninachagua kuwa na uhusiano mzuri na Mungu na kuwa tayari kumtumikia kila wakati."

## MASWALI NA MAJIBU - SOMO LA 6

1. Je, ni hali gani ambayo unaweza kuhitajika kushiriki injili ghafla, bila kujiandaa mapema?
Mifano: Mtu anayeketi karibu nawe kwenye treni anauliza maswali kuhusu Biblia. Rafiki yako ana mfadhaiko wa mawazo na anafikiria suhulu ni kufa tu. Mwalimu wako shuleni anasema Mungu haishi.
2. Je, ungefundisha somo gani ikiwa ingekulazimu uongoze darasa?
Ni swali nzuri kwa wanafunzi kufikiria kuhusu iana ya masomo katika biblia ambayo wangefundisha. Katika historia yote Mungu ametumia watu kuzungumza na watu wengine wa rika lao.
3. Je, tofauti ya injili ya "AMANI" na injili ya woga ni nini?
Kwa kweli, injili inasema kwamba wokovu ndiyo njia pekee ya kuepuka kuungua kuzimu milele.  Watu wanaogopa kufa, na wako tayari kusikiliza injili kwa sababu ya woga huo.  Ni kweli pia ikiwa tunawasilisha injili kama njia bora ya kuishi.  Tunaweza kupata amani bila kujali kinachotokea maishani yetu.  Tunaweza kuona upendo wa Mungu katika maisha yetu.
4. Je, Mhabeshi alimuuliza Filipo nini?
Aliuliza maana ya maandiko aliyokuwa anasoma.
5. Mhabeshi alipoona maji, aliomba nini?
Ubatizo

## MCHEZO: ULINZI - SOMO LA 6



### NYENZO

Utepe wa kufunga au uzi

### MAANDALIZI

Weka alama ya mistari miwili sambamba kwa kutumia utepe, iwe takriban mita sita kutoka kwa mwingine, na mita tatu kwa upana.

### KUCHEZA MCHEZO

Chagua mwanafunzi ambaye atakuwa amesimama kati ya mistari wakati wengine wanakimbia. Na kila mwanafunzi atakaoweza kugusa anapaswa kusimama mahali alipo kama amegandishwa, na atasalia pale kama amegusa kichwa chake, mabega, magoti na miguu. Watoto wanaokimbia lazima wawe waangalifu ili wasiguswe na kugandishwa, lakini wanaweza kugusa mwanafunzi mwingine aliyegandishwa ili kuwaokoa na anendelee kukimbia pamoja na wengine.
Wanapofikia katika mstari, lazima wasubiri ishara ya kurudi kwenye mstari huo mwingine ili waendelee na mchezo kwa kubadilisha mwanafunzi aliyeteuliwa na kuweka mjitoleaji mwingine.


## CHAGUO


Kila wakati unapobadilisha mwanafunzi ambaye atakuwa amesimama kati ya mistari, unaweza pia kurekebisha maagizo ambayo yatatekelezwa na mwanafunzi huyo.

Moja ya maagizo haya inaweza kuwa kupiga vidole au aendelee kutembeatembea kama askari katika sehemu moja.

## MAJIBU YA FUMBO - SOMO LA 6

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| R | O | H | A | M | T | O | W | A | S | H | I |
| M | Y | P | E | T | R | O | R | A | S | S | K |
| H | B | E | I | R | I | F | A | S | A | T | U |
| A | A | O | R | L | L | S | F | R | M | Z | B |
| B | R | H | I | U | I | A | A | W | A | A | A |
| E | A | O | L | M | S | F | D | Z | N | K | T |
| S | B | R | S | W | A | A | I | L | I | I | I |
| H | A | A | E | L | M | T | L | I | A | D | Z |
| I | R | F | I | B | Z | B | A | E | B | N | W |
| P | A | R | O | N | H | T | I | R | M | A | A |
| O | A | B | U | K | D | R | K | Z | A | U | N |
| G | A | K | I | R | I | B | U | H | U | K | R |







# SOMO LA 7

## KICHWA - SOMO LA 7
Ngao ya imani

## HADITHI YA BIBLIA – SOMO LA 7
Paulo na meli iliyovunjika
Matendo 27:21-37, 28:1

## ALAMA ZA CHEO - SOMO LA 7






Alama za Cheo za Mahudhurio ya leo:
Kila mwanafunzi aliyeshiriki katika "kambi ya mazoezi" ya wiki iliyopita anapokea "riboni" hii:




Kila mwanafunzi aliyemaliza shughuli ya kusoma kwa wiki iliyopita kutoka kwa kitabu cha Matendo anapokea nyota.

Kila mwanafunzi anayeweza kukariri mstari wa kumbukumbu wa wiki iliyopita anapokea nyota.

## MCHEZO WA KUIGIZA – SOMO LA 7
Leo Sajenti Mlingoti anawapa askari Mcheko na Zamu ngao mpya. Katika mazoezi, askari wanatumia ngao ili kujilinda kutokana na maji yanayorushwa kwenye uwanja. Askari Zamu anakuwa hodari kwa kutumia ngao yake na anamaliza uwanja akiwa tu amepata maji kidogo katika mavazi yake. Mcheko alisahau ngao yake kabisa na analowa maji kabisa.


## MSTARI WA KUMBUKUMBU – SOMO LA 7
"zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu." Waefeso 6:16

## SOMO KUU - SOMO LA 7
**Matendo 27:21-37, 28:1**

Leo tunajifunza kuhusu ngao ya imani, silaha yenye umuhimu kwa ajili ya kujilinda kwa sababu tunaweza kuizungusha na kujikinga na shambulio fulani. Bibilia inasema kwamba tunaweza kuitumia ili kujizuia mishale ya moto ya yule mwovu. Haisemi "ikiwa" mishale itakuja, lakini inasema "wakati" itakapokuja, tutakuwa na nguvu ya kujilinda. Ukweli ni kwamba adui anatuvamia kila wakati. Adui yako anataka kukuvuruga kwa kutumia mishale ya moto na kukutia hofu. Amebuni mkakati wake maalum kwa ajili yako. Amechambua mazoea yako, hofu yako ya kina na udhaifu wako, na analenga mishale yake katika maeneo hayo haswa. Imani ni kumwamini Mungu na Neno lake, hata ingawa hatuwezi kuuona ufalme wake wa kiroho. Tunajua kuwa Mungu yuko ingawa hatuwezi kumwona, na hiyo ni imani mioyoni mwetu. Kwa sababu tunayo imani, tunaweza kushinda shambulio hili la maadui.
Katika hadithi ya leo ya Bibilia kutoka kitabu cha Matendo, Paulo alikuwa baharini wakati wa dhoruba kali, na Mungu akamwambia kwamba hakuna mtu atakayeangamia ndani ya meli kutokana na dhoruba hiyo! Paulo alichagua kuamini kuwa ni Mungu aliyekuwa amezungumza naye, ingawa hakuweza kumwona Mungu.

Inafurahisha kuona kwamba Paulo akiwaambia watu kile Mungu alisema, na answaambia wale chakula kikubwa ili kupata nguvu. Paulo hakumwamini Mungu tu, lakini alikuwa tayari kushiriki hadharani ujumbe wa Mungu na wengine na kuchukua hatua kulingana na ujumbe huo! Angeaibika sana ikiwa mtu angeangamia kutokana na kuanguka kwa meli.Wakati mwingine pia tunahitaji kutangaza hadharani Neno la Mungu, tukimwamini Yeye badala ya wanadamu. Je, utachukua ngao yako ya imani na kuamini mambo usiyoyaona? Hivi ndivyo utakavyoshinda dhidi ya adui na kuzima mishale yake ya moto!

## KAMBI YA MAZOEZI - SOMO LA 7



### KAZI YA ZIADA – SOMO LA 7

Wiki hii andika orodha ya mambo unayoamini kutoka kwa Bibilia ingawa hayaonekani, lakini unayaamini hata hivyo. Ni gani kati ya orodha yako ambayo adui atatumia ili kukushambulia haswa?

### KAZI YA NYUMBANI (WANAFUNZI WAKUBWA) - SOMO LA 7

Soma Matendo 20-22

## POWERPOINT / UAMUZI - SOMO LA 7

"Nachagua kumwamini Mungu na kuwa na imani."

## MASWALI NA MAJIBU - SOMO LA 7

1. Katika maisha halisi, "mishale ya moto ya yule mwovu" ni migani?
Mifano: Mwalimu wako anasema kwamba mwanadamu alitokana na tumbili na kwamba Mungu sio muumba wa vitu vyote. Wengine wanasema kwamba Yesu alikuwa mtu mzuri tu na sio Mungu. Unaogopa kwamba Mungu hawezi kubadilisha maisha ya wazazi wako.
2. Je, ni mfano mgani maalum wa jinsi unavyoweza kukwepa mshale kwa kutumia ngao yako ya imani katika maisha halisi?
Unaposikia kwamba Mungu hakuumba ulimwengu, unafungua Biblia yako na kusoma Mwanzo 1 na 2 ili kujikumbusha kile kilichotokea.
3. Je, unafanya nini ili kuhakikisha hautaondoka nyumbani bila imani yako?
Bibilia inasema kwamba imani huja kwa kusikiliza Neno la Mungu.Tunahitaji kusoma na kusikia Neno la Mungu mara kwa mara na kukariri mafungu, kwa njia hii tutakuwa na ngao ya imani kila wakati. Pia, unapoamua kuamini kile Mungu anachosema badala ya kile wengine wanachosema, unadhihirisha imani.
4. Je, Paulo alikuwa akienda wapi alipokuwa safarini katika hadithi ya leo ya Bibilia? Kulikuwa na watu wangapi katika meli hiyo?
(276) Italia. Onyesha ramani na miji na bandari ambazo alitembelea wakati wa safari hii. (Sidoni, Patara, Knidasi, Lasea, Krete, Kauda, Malta)
5. Je, Paulo alijuaje kwamba meli ingeharibika lakini hakuna mtu angeangamia kwa sababu ya dhoruba?
Malaika alikuja na kumwarifu. Matendo 27: 23-25

## MCHEZO: NGAO - SOMO LA 7

### NYENZO

Utepe wa kufunga, sanduku la kadibodi, na karatasi ya rangi.



### MAANDALIZI

Tumia utepe wa kufunga ili kuunda mraba kwenye sakafu ya mita moja na nusu kila upande na uweke sanduku kwenye Katikati.

### KUCHEZA MCHEZO

Gawanya kikundi chako katika timu nne na uunde mipira ya karatasi ya rangi tofauti. Watoto wanasimama nje ya mraba mkubwa na kujaribu kutupa mipira ya karatasi ndani ya sanduku. Kila timu inachagua mwakilishi ambaye atakuwa akizunguka ndani ya mraba mkubwa, akijaribu kuzuia mipira ya karatasi ya timu pinzani isiingie katika sanduku. Mwishowe mwanafunzi atahesabu mipira ya

karatasi kwenye sanduku la kadibodi kwa kuzitenganisha kulingana na rangi. Timu ambayo imekusanya nyingi inakuwa washindi.

## MAJIBU YA FUMBO - SOMO LA 7

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| K | M | U | K | I | S | U | A | M | A | S | I |
| T | U | A | W | U | L | H | U | W | B | M | Y |
| O | S | O | K | Z | S | G | E | G | A | B | N |
| F | H | G | K | I | H | H | S | N | H | G | L |
| A | A | Z | A | O | A | A | I | W | A | Y | O |
| U | U | M | M | Y | L | L | R | O | R | Z | L |
| T | R | S | I | U | E | E | A | S | I | K | U |
| I | I | L | U | M | B | H | W | M | G | U | A |
| M | A | B | A | H | A | R | I | A | W | K | P |
| H | O | H | R | Z | B | H | U | L | U | I | S |



# SOMO LA 8

## KICHWA - SOMO LA 8
Helmeti ya wokovu

## HADITHI YA BIBLIA – SOMO LA 8
Kubadilika kwa Sauli
Matendo 9:1-19

## ALAMA ZA CHEO - SOMO LA 8

Alama za Cheo za Mahudhurio ya leo:
Kila mwanafunzi aliyeshiriki katika "kambi ya mazoezi" ya wiki iliyopita anapokea "riboni" hii:




Kila mwanafunzi aliyemaliza shughuli ya kusoma kwa wiki iliyopita kutoka kwa kitabu cha Matendo anapokea nyota.

Kila mwanafunzi anayeweza kukariri mstari wa kumbukumbu wa wiki iliyopita anapokea nyota.




## MCHEZO WA KUIGIZA – SOMO LA 8
Askari Mcheko anaingia akiwa amevaa mavazi yake yote isipokuwa helmeti. Akiwa na wasiwasi, Askari Zamu anauliza helmeti ya Mcheko iko wapi. Mcheko anasema kwamba kwa sababu ana mavazi mengine yote, amelindwa vya kutosha na hahitaji helmeti Wakati wa mafunzo, anaendelea kugongwa kwenye kichwa chake. Sajenti Mlingoti anamkumbusha kuwa vifaa vingine havitoshi - anahitaji helmeti pia!

## MSTARI WA KUMBUKUMBU – SOMO LA 8
"Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu" Waefeso 6: 17a

## SOMO KUU - SOMO LA 8
**Matendo 9:1-19**

Ni muhimu kuvaa helmeti zetu za wokovu kwa sababu inaweza kuwa hatari ikiwa tutagongwa kichwani. Je, tutahakikisha vipi kuwa tumevaa helmeti zetu? Biblia inaweka wazi kuwa wokovu wetu unategemea kazi iliyomalizika ya Yesu Kristo msalabani. Alipokufa kwa ajili ya dhambi zetu, alilipa gharama na akanunua wokovu wetu! Hatuwezi kuingia mbinguni kwa matendo mema, lakini kwa kumwamini Yesu Kristo tu, njia pekee ya wokovu. Hatuhitaji kuwa na sherehe za maombi kila siku ili tuweze kuvaa helmeti zetu za wokovu. Ikiwa tumemwamini Bwana Yesu Kristo kwa wokovu wetu, basi tumevaa helmeti zetu!
Mungu alimtokea Sauli kwa njia ya kimiujiza katika hadithi ya leo ya Bibilia kutoka kitabu cha Matendo. Sauli, ambaye baadaye anabadilika kuwa Paulo, alikuwa anawadhihaki na kuwatesa Wakristo. Siku moja akielekea Dameski, Yesu alimtokea Sauli kwa ghafla kama mwangaza kutoka mbinguni na Sauli akaanguka chini na kupoteza uwezo wa kuona. Siku tatu baadaye, Mungu alimtuma Mkristo ili kumponya na kumleta kwa Kristo. Wiki hiyo Sauli alimwamini Yesu na akaokolewa! Unaweza kuvaa helmet yako ya wokovu leo, jinsi Paulo alivyofanya, ikiwa utaomba na kumwamini Bwana Yesu Kristo kwa wokovu wako.

Omba nami, "Bwana Yesu, leo nakubali kuwa mimi ni mwenye dhambi na nimekosa. Ninaamini kuwa ulikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zangu na kwamba unaishi. Ninakubali moyoni mwangu leo uwe Bwana na Mwokozi wangu. Asante kwa kunipokea, kunipenda, na kunipa uzima wa milele na wewe mbinguni!"

## KAMBI YA MAZOEZI - SOMO LA 8

### KAZI YA ZIADA – SOMO LA 8



Andika kwenye ukurasa wa kwanza wa bibilia yako mahali ambapo uliomba ili kuokolewa. Ikiwa huwezi kukumbuka, unaweza kuifanya hili hivi sasa! Nenda mahali maalum (chumbani mwako, nyuma ya nyumba yako, au kanisani) na umwombe Mungu akusamehe. Mshukuru Yesu kwa kulipia dhambi zako na maisha yake, na umuombe awe bwana na mwokozi wako. Mwambie unataka kuishi kwa ajili Yake. Andika wakati na mahali kwenye ukurasa wa mbele wa Bibilia yako au kwenye kitabu chako cha mwanafunzi.

### KAZI YA NYUMBANI (WANAFUNZI WAKUBWA) - SOMO LA 8

Soma Matendo 23-25

## POWERPOINT / UAMUZI - SOMO LA 8

"Nachagua kumtumaini Bwana Yesu kwa wokovu wangu."

## MASWALI NA MAJIBU - SOMO LA 8

1. Je, unaweza kuwa na uhakika wa wokovu wako?
Kila mwanafunzi anapaswa kujibu swali hili na atoe sababu ya kwa nini. Wazo ni wao kufahamu kuwa ikiwa watamkubali Yesu mioyoni mwao kama Mwokozi wao, tayari wamepokea wokovu.
2. Je, unafikiria unaweza kupoteza wokovu wako?
Kuna mitazamo tofauti, wengine hufikiria kuwa inawezekana, kwamba wanaweza kupoteza wokovu wao na wengine ambao hawaamini hilo. Wazo ni kwa wanafunzi kujadili majibu yao.
3. Je, ni nini kilimfanyikia Sauli alipokuwa akiendesha farasi wake kwenda katika mji wa Dameski?
Mwanga mkali kutoka Mbingu ulikuja na akaanguka chini na akawa kipofu. Mungu alizungumza naye moja kwa moja. (Matendo 9)
4. Je, Mungu alimwambia Anania wa Dameski nini?
Mungu alimwambia aende kumwombea Sauli. Alimwambia kuhusu hitaji la uponyaji la Sauli na mahali angepata nyumba alimokuwa Sauli.
5. Anania alimwambia Mungu nini? Je, nini hutendeka tunapomlalamikia Mungu?
Anania alisema, "Nimesikia kuhusu umbaya ambao Sauli amewatendea Wakristo. Ana mamlaka hata katika mji huu wa kutufunga." Mungu alikuwa na uvumilivu kwa Anania.

## MCHEZO: MKAKATI - SOMO LA 8

### KUCHEZA MCHEZO



Chagua mwanafunzi kuwa mtangazaji. Kuanza mchezo, wanafunzi wanaanza kutembea kuzunguka chumba. Wakati mtangazaji anasema, "Kuna Wokovu!" wanafunzi wanaacha kutembea, wanazunguka mara moja mahali walipo, na kuketi chini haraka iwezekanavyo. Mwanafunzi wa kwanza kuketi anapaswa aseme kitu kuhusu Yesu Kristo na kisha inakuwa zamu yake kuwa mtangazaji. (Ikiwa mwanafunzi anayeshinda tayari amekuwa mtangazaji, mwambie achague mwanafunzi mwingine ambaye hajakuwa mtangazaji)


### CHAGUO

1. Kila wakati unapocheza, unaweza kubadilisha maagizo unayotoa kwa wanafunzi. (Mfano, weka mikono yako kichwani na kuzunguka mahali ulipo kisha uketi, ruka kwa mguu mmoja mara mbili, kimbilia ukuta ulio karibu, nk.)

2. Ikiwa ni vigumu sana kutambua mshindi, maelezo mengine yanaweza kutumiwa ili kuchagua mtangazaji - mwanafunzi aliyevaa mavazi ya bluu, mwanafunzi mdogo kabisa, mwanafunzi aliye na jina ndefu zaidi la familia, nk.
3. Mtangazaji anaweza kusema kwa sauti "Kuna Wokovu" huku akipiga makofi, au kupiga filimbi, au unaweza kutumia muziki na kisha kuusimamisha.

## MAJIBU YA FUMBO - SOMO LA 8



| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| W | U | O | M | I | K | I | S | P | F | A |
| V | M | P | K | B | K | O | A | O | W | U |
| R | O | H | O | S | I | N | U | I | Y | W |
| U | V | U | E | F | W | N | L | Z | E | O |
| M | Y | M | A | U | U | U | G | N | S | N |
| U | A | E | S | I | G | L | U | U | A | O |
| D | S | C | S | A | N | S | I | F | N | K |
| I | N | A | H | U | K | A | M | A | G | I |
| A | N | C | U | O | M | A | N | N | U | M |
| N | U | A | I | L | A | C | H | A | V | O |
| K | U | H | A | N | I | M | A | W | U | V |

# SOMO LA 9

## KICHWA - SOMO LA 9
Upanga wa Roho

## HADITHI YA BIBLIA – SOMO LA 9
Petro ahubiria umati
Matendo 2:12-17, 22-30, 34-41

## ALAMA ZA CHEO - SOMO LA 8
Alama za Cheo za Mahudhurio ya leo:
Kila mwanafunzi aliyeshiriki katika "kambi ya mazoezi" ya wiki iliyopita anapokea "riboni" hii:




Kila mwanafunzi aliyemaliza shughuli ya kusoma kwa wiki iliyopita kutoka kwa kitabu cha Matendo anapokea nyota.

Kila mwanafunzi anayeweza kukariri mstari wa kumbukumbu wa wiki iliyopita anapokea nyota.

## MCHEZO WA KUIGIZA – SOMO LA 9
Zamu amweleza Mcheko kuhusu mapambano kadhaa ya kibinafsi, na Mcheko anampa ushauri. Zamu anamuuliza Mcheko alipopata mawazo kama hayo. Mcheko anatoa simu yake ya mkononi, akisema alitoa katika mitandao ya kijamii. Wakati huo huo, Sajenti Mlingoti anaingi ana anawamba wamsikilze kwa umakini, akiwaambia kwa wanapaswa kutegemea Bibilia na sio mitandao ya kijamii. Askari Zamu na Mcheko wanaanza kusoma Bibilia, na kila mmoja anapokea upanga wake kutoka kwa biblia!

## MSTARI WA KUMBUKUMBU – SOMO LA 9
"Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu" Waefeso 6: 17b

## SOMO KUU - SOMO LA 9
**Matendo 2:12-17, 22-30, 34-41**

Upanga wa roho ni kipande cha kwanza cha Silaha ambayo ni silaha halisi, badala ya kifaa cha kujilinda. Hii inamaanisha kuwa tunaweza kumshambulia adui kwa kutumia upanga. "Upanga wa Roho" ni Bibilia, au Neno la Mungu. Ili uweze kutumia upanga wako vitani, unahitaji kufahamu Maandiko. Hii inamaanisha kusoma bibilia yako tena na tena na pia kukariri mafungu ya Bibilia.
Katika hadithi ya kweli ya leo kutoka kwenye kitabu cha Matendo, Petro anatumia maandiko wakati anahubiria umati wa watu. Kuna watu waliokuwa pale ambao hawakumwamini Mungu na wakaanza kumdhihaki. Petro alisimama na kuhubiria wale waliomdhihaki; hakuhubiri tu, lakini alitumia maandiko kupigana vita. Tunapokuwa tumekariri maandiko vizuri, tunaweza kuyatumia maishani wakati tunapohitaji. Siku hiyo watu elfu tatu waliokolewa na kujiunga na kanisa hilo kwa sababu Petro alitumia mahubiri kutoka kwa Neno la Mungu! Ilikuwa baraka ya kufana! Petro alitumia upanga wake kwa ustadi kwa sababu alikuwa amekariri maandiko kwa ajili ya hali hii mahususi. Alipigana na adui kwa ustadi na akawaleta watu 3000 katika

upande wa Bwana! Jinsi unavyofahamu mafungu mengi ya biblia, ndivyo unavyokuwa hodari zaidi katika kutumia upanga wako. Tunaposoma Neno na kulikariri, Mungu anatuwezesha kulikumbuka tunapolihitaji. Je, unatumia vipi upanga wako?

## KAMBI YA MAZOEZI - SOMO LA 9

### KAZI YA ZIADA – SOMO LA 9



Kariri fungu la Bibilia ambalo linatumika katika vita ambavyo unapigana mara kwa mara na umweleze mwalimu wako wiki ijayo. Unaweza kuwa una hofu kuhusu muonekano wako, mali, kutaka mambo zaidi, usalama wa kiroho, au maisha yako ya baadaye.

### KAZI YA NYUMBANI (WANAFUNZI WAKUBWA) - SOMO LA 9

Soma Matendo 26-28

## POWERPOINT / UAMUZI - SOMO LA 9

"Nachagua kujifunza Neno la Mungu na kulitumia katika maisha yangu ya kila siku."

## MASWALI NA MAJIBU - SOMO LA 9

1. Je, ni wakati gani unaweza kumshambulia adui?
Kuombea wokovu wa wengine, kutangaza ahadi za Bibilia, kumsifu Mungu, nk.
2. Je, ni mfano gani unadhihirisha matumizi ya upanga katika maisha halisi?
Mfano: Unasikia uwongo kutoka kwa shetani (mtu anakuambia kuwa hupendezi) na mara moja unakumbuka mstari kutoka kwa Bibilia unaosema kuwa wewe ni mtu wa pekee kwa Mungu na uumbaji wake.
3. Je, watu hutumia upanga wa roho kwa njia ipi isiyofaa?
Wakati Wakristo wanasahau kwamba uhakika unatokana na Roho Mtakatifu, na wanatumia vifungu vya Bibilia kushambulia Wakristo wengine. Wakati Roho Mtakatifu anapokuhukumu kwa dhambi, Yeye anakupa nguvu na usaidizi wa kuishi ili kumpendeza.
4. Je, ni watu wangapi waliokoka kwa sababu ya mahubiri ya Petro katika Yerusalemu siku ya Pentekosti?
Karibu 3,000
5. Je, Wakristo hawa wapya walifanya nini ili kuonyesha kuwa wangefuata Kristo?
Walibatizwa.

## MCHEZO: MSIMBO - SOMO LA 9

### NYENZO

Vipande kadhaa vya barafu kavu, sahani zinazoweza kutupwa.


### KUCHEZA MCHEZO



"Je, unadhani ni njia ipi bora ya kupeleka barafu kavu hadi upande mwingine wa chumba bila kutumia mikono yako? Kila siku tunafanya maamuzi kuhusu njia bora ya kufanya na kusema mambo. Mungu anaahidi kutusaidia katika maamuzi haya - tunapokariri na kufanya mazoezi ya mafungu hayo kutatupa usaidizi."

1. Onyesha (au uombe wasaidizi waonyeshe) njia tofauti za kuhamishaa barafu kavu hadi upande wa pili wa chumba bila kutumia mikono yako... na kutumia tu sahani kama feni. (kwa kusonga polepole au kupiga hatua ndefu, nk.)
2. Weka wanafunzi katika vikundi visivyozidi wanafunzi 6. Vikundi vimewekwa kwa safu katika upande mmoja wa eneo la kucheza. Mpe mtoto wa kwanza katika kila safu sahani na kipande cha barafu kavu.
3. Wakati mwalimu anasema, watoto wa kwanza waanze kuhamisha barafu kavu upande wa pili bila kutumia mikono yao. Wanapofika kwenye ukuta wa upande mwingine, wanainua barafu kavu kwa mikono yao, na wanakimbia kurudi ili kupeleka sahani kwa mwanafunzi anayefuata.

## MAJIBU YA FUMBO - SOMO LA 9



| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| W | Y | K | P | R | M | R | O | H | O | I | Y |
| R | A | H | U | O | A | R | A | Y | Y | D | E |
| M | Z | K | S | F | T | H | O | M | O | U | R |
| A | I | U | O | E | U | M | A | I | S | H | A |
| T | J | F | P | P | M | F | W | A | Y | A | S |
| U | U | M | E | L | A | S | U | R | E | Y | A |
| M | I | U | W | J | I | Z | A | K | S | A | L |
| A | M | F | U | G | N | U | M | R | A | W | E |
| I | R | U | A | M | I | U | J | I | S | A | M |

# SOMO LA 10


## KICHWA - SOMO LA 10
Kuomba bila kukoma

## HADITHI YA BIBLIA – SOMO LA 10
Peter aachiliwa gerezani
Matendo 12:1-19

## ALAMA ZA CHEO - SOMO LA 10




Alama za Cheo za Mahudhurio ya leo:
Kila mwanafunzi aliyeshiriki katika "kambi ya mazoezi" ya wiki iliyopita anapokea "riboni" hii:




Kila mwanafunzi aliyemaliza shughuli ya kusoma kwa wiki iliyopita kutoka kwa kitabu cha Matendo anapokea nyota.

Kila mwanafunzi anayeweza kukariri mstari wa kumbukumbu wa wiki iliyopita anapokea nyota.
Katika wiki hii ya mwisho, kila mwanafunzi anaweza kupata riboni ya 10 ya kazi ya nyumbani kwa kuamua kufanya kazi ya nyumbani na kuomba leo. Ikiwa wamekamilisha shughuli zote 9 za kusoma, wanapata nyota yao ya 10 ya kusoma. Ikiwa wanaweza kukariri vifungu vyote vya kumbukumbu kwa mfululizo ikiwa ni pamoja na fungu la siku ya leo, wanapata nyota yao ya 10 ya kumbukumbu.




## MCHEZO WA KUIGIZA – SOMO LA 10
Sajenti Mlingoji anatoa redio ya mawasiliano kwa Askari Mcheko na Zamu. Katikati ya mazoezi ya hali ya juu ya mafunzo, Mcheko na Zamu wanakwama ndani ya shimo. Zamu anapendekeza watumie redio ya mawasiliano ili kuomba usaidizi. Mcheko anakataa mara ya kwanza, akidai kwamba wana uwezo wa kujiokoa. Baada ya muda, wanawasha redio ya mawasiliano na kumlilia Mungu. Sajenti Mlingoti anatokea ghafla katika sehemu hio na anamfukuza adui.

## MSTARI WA KUMBUKUMBU – SOMO LA 10
"kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote" Waefeso 6:18


## SOMO KUU - SOMO LA 10
**Matendo 12:1-19**

Maombi ni silaha ya pili ambayo tunaweza kutumia ili kumshambulia adui. Na pia yanaweza kutumika kama kinga. Kwa maombi tunaweza kupigana vita, kupokea hekima kutoka kwa Bwana kuhusu jinsi ya kuendelea, kuachilia malaika mbinguni kutupigania, na kuelewa vizuri adui yetu.

Katika hadithi ya leo ya bibilia, tunaona Petro akiwa gerezani wakati kanisa lote lilikuwa likimuombea. Wakati wanaomba, Mungu anatuma malaika gerezani na kumwachilia Petro! Malaika anamwongoza nje ya gereza, kwenye barabara na Petro anarudi nyumbani ambapo ndugu na dada katika Kristo wanaomba. Walikuwa wanakataa kumfungulia mlango kwa sababu hawakuwa wana uhakika ni yeye! Walikuwa wakiombea wokovu wake, lakini walishangaa kuona miujiza ikitendeka! Mara nyingi, wewe na mimi huwa tunaomba, lakini tunashangaa wakati Mungu anajibu maombi yetu na anapotusaidia.Anatuelekeza tuwe tunamwomba na anaahidi kutusaidia. Hii ni sehemu moja ya Silaha ambayo lazima utekeleze kila siku ikiwa unataka kuitumia kila siku. Maombi hubadilisha mambo! Omba kila wakati katika vita vyako kwa sababu tunahitaji maombi katika vita leo zaidi ya jana.

## KAMBI YA MAZOEZI - SOMO LA 10

### KAZI YA ZIADA – SOMO LA 10



Tabia huchukua marudio 21 kila kila siku ili kuwa mazoea. Anza kuomba kila jioni unapopanda kitandani. Ni sawa hata ikiwa ni maombi mafupi, lakini sio sawa ukikosa hata siku moja. Ikiwa unakosa kuomba katika siku fulani, omba mara mbili asubuhi kwa urefu mara dufu baada ya kuamka. Badilisha kitanda chako kuwa mahali pako pa maombi. Jipatie tuzo unapofikia siku 21 za maombi.

### KAZI YA NYUMBANI (WANAFUNZI WAKUBWA) - SOMO LA 10

Hakuna shughuli ya kusoma wiki hii

## POWERPOINT / UAMUZI - SOMO LA 10

"Nachagua kuomba kila wakati, nikikumbuka kuwa vita ni vya kiroho."

## MASWALI NA MAJIBU - SOMO LA 10

1. Je, kwa nini maombi yamejumuishwa kama sehemu ya "Silaha ya Mungu"?
Maombi yanaweza kukuimarisha wewe au marafiki zako, na maombi yana uwezo wa kubadilisha mawazo ya Mungu na ya adui zako.
2. Je, ni mfano gani wa maombi ya kujilinda dhidi ya adui na ni mfano gani wa maombi ya kushambulia adui?
Ulinzi: Maombi ili upate ujasiri au kuomba msaada. Pia, tambua kuwa kuambiwa uwongo au kutusiwa ni mojawapo ya shambulio la kiroho. Kataa kuingia katika majaribuni kwa jina la Yesu Kristo.
Shambulio: Kuombea wengine waokolewe, kuombea jiji liweze kumjua Kristo, au kuomba dhidi ya sanamu fulani au miungu katika eneo lako.
3. Ikiwa Mungu ana udhibiti wa kila kitu, kwa nini Anatuuliza tumwombe wakati tayari anajua kitakachotokea?
Kwa sababu wewe unasaidia kuamua nini kitakachotokea. Maombi yako yanaleta mabadiliko katika maisha yako na maisha ya walio karibu nawe.
4. Je, ni silaha gani mbili za mashambulizi tunaweza kutumia?umia?
Maombi na Upanga wa Roho, ambao ni Neno la Mungu.
5. Je, ni nani aliyekuja mlangoni wakati Petro alibisha nyumbani kwa Mariamu?
Rhoda, msichana mtumishi

## MCHEZO: SHAMBULIZI - SOMO LA 10

### UTANGULIZI



Tunatumia maombi ili kujilinda na kushambulia. Pia, katika mchezo huu tunapaswa kusonga mbele ili kukusanya karatasi, wakati huo huo tunapaswa kulinda mgongo wetu wenyewe.

### NYENZO

Karatasi (karatasi za ukubwa wa herufi zilizokatwa katika miraba 4 - robo moja kwa kila mwanafunzi katika darasa lako), utepe.

## KUCHEZA MCHEZO

1. Weka karatasi kwenye mgongo wa kila mwanafunzi.
2. Mwalimu anapoelekeza, wanafunzi wanajaribu kunyakua karatasi kutoka kwa migongo ya wanafunzi wengine. Wanafunzi hawawezi kugusa karatasi katika mgongo wao ili kuizuia. Lakini wanapaswa kutoroka ili wengine wasiibe karatasi yao ndogo.
3. Wakati mwanafunzi anachukua karatasi ya mwanafunzi mwingine, mwanafunzi anapaswa kumpa mwanafunzi huyo karatasi zote ambazo amekusanya, na anapaswa arudi ukutani ili kuanza tena.
4. Endelea hadi kuwe mwanafunzi mmoja tu katikati na karatasi zote. Sambaza tena makaratasi na kucheza tena.

## CHAGUO

Badala ya karatasi na utepe, unaweza kutumia vipande vya nguo ambazo ni ndefu na nyembamba, na wanafunzi waziweke katika mishipi yao.


## MAJIBU YA FUMBO - SOMO LA 10

Yafuatayo ni mawazo. Kubali majibu anuwai.


Omba kwa: familia, chakula, kanisa, magonjwa, hekima.

Mfano wa ombi: Asante Mungu Baba kwa siku moja zaidi maishani na familia yangu yote. Tafadhali msaidie baba yangu. Amina. (Kubali majibu anuwai)

Vitu vinavyofanya iwe ngumu kuomba: Kuhisi kulala, kupata shughuli nyingi na marafiki, kuamka kama umechelewa, kazi za nyumbani na kusaidia kusafisha nyumba.




| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| P | L | B | G | A | Z | P | E | T | R | O |
| D | E | O | Y | E | K | A | N | I | S | A |
| I | Z | T | R | U | R | I | K | A | J | E |
| H | H | E | R | O | D | E | A | N | M | M |
| S | E | M | L | U | R | E | Z | L | H | U |
| E | R | L | H | G | D | O | A | A | A | O |
| J | O | A | B | N | L | F | Y | G | O | M |
| A | Y | N | L | U | M | A | O | N | O | B |
| M | D | G | O | M | F | A | L | M | I | A |
| M | I | O | N | Y | O | R | O | Y | A | M |



# CHATI YA DARASA LANGU

| ALAMA ZA CHEO NA UTOFAUTI | (Somo la 1) | (Somo la 2) | (Somo la 3) | (Somo la 4) | (Somo la 5) | (Somo la 6) | (Somo la 7) | (Somo la 8) | (Somo la 9) | (Somo la 10) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwanafunzi: | | | | | | | | | | | Mahudhurio |
| | | | | | | | | | | | Kusoma |
| | | | | | | | | | | | Kukariri |
| | | | | | | | | | | | Kazi ya nyumbani |
| Mwanafunzi: | | | | | | | | | | | Mahudhurio |
| | | | | | | | | | | | Kusoma |
| | | | | | | | | | | | Kukariri |
| | | | | | | | | | | | Kazi ya nyumbani |
| Mwanafunzi: | | | | | | | | | | | Mahudhurio |
| | | | | | | | | | | | Kusoma |
| | | | | | | | | | | | Kukariri |
| | | | | | | | | | | | Kazi ya nyumbani |
| Mwanafunzi: | | | | | | | | | | | Mahudhurio |
| | | | | | | | | | | | Kusoma |
| | | | | | | | | | | | Kukariri |
| | | | | | | | | | | | Kazi ya nyumbani |
| Mwanafunzi: | | | | | | | | | | | Mahudhurio |
| | | | | | | | | | | | Kusoma |
| | | | | | | | | | | | Kukariri |
| | | | | | | | | | | | Kazi ya nyumbani |
| Mwanafunzi: | | | | | | | | | | | Mahudhurio |
| | | | | | | | | | | | Kusoma |
| | | | | | | | | | | | Kukariri |
| | | | | | | | | | | | Kazi ya nyumbani |
| Mwanafunzi: | | | | | | | | | | | Mahudhurio |
| | | | | | | | | | | | Kusoma |
| | | | | | | | | | | | Kukariri |
| | | | | | | | | | | | Kazi ya nyumbani |
| Mwanafunzi: | | | | | | | | | | | Mahudhurio |
| | | | | | | | | | | | Kusoma |
| | | | | | | | | | | | Kukariri |
| | | | | | | | | | | | Kazi ya nyumbani |
| Mwanafunzi: | | | | | | | | | | | Mahudhurio |
| | | | | | | | | | | | Kusoma |
| | | | | | | | | | | | Kukariri |
| | | | | | | | | | | | Kazi ya nyumbani |
| Mwanafunzi: | | | | | | | | | | | Mahudhurio |
| | | | | | | | | | | | Kusoma |
| | | | | | | | | | | | Kukariri |
| | | | | | | | | | | | Kazi ya nyumbani |

Unda nakala za ukurasa huu ikiwa una zaidi ya wanafunzi 10